SUPA JACKPOT
TZS.1,027,393,141
KWA TZS.1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
*150*87#



UKURASA 3

**BUNGE** lanusa harufu ufisadi wa mabilioni ya manispaa




UKURASA 11

Nipashe
Jumamosi Septemba 3, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581057
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper

# Tozo mpya benki, simu zamwibua Kitwanga

**AMKOSOA** Waziri Mwigulu, amwita mezani ampe...

*Endelea ukurasa wa 2*



Dk. Mwigulu Nchemba

Charles Kitwanga

## Abiria wakaa saa 3 baharini upepo ukiipiga MV Magogoni

UKURASA 2



Pantoni ya MV Magogoni, ikiwa imekwama ufukweni mwa Bahari ya Hindi jijini Dar es Salaam baada ya kusukumwa na upepo kutoka kwenye lango lake la kupakia abiria la Magogoni Feri jana. **PICHA: ROMANA MALLYA**

UKURASA WA 3

## TMA YATABIRI UPUNGUFU WA MVUA ZA VULI

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imetabiri kuwapo upungufu mkubwa wa mvua za vuli katika mikoa inayopata mvua mara mbili kwa...

## DC aanika madudu ya kutisha serikalini

UKURASA 3

**MICHEZO** **YANGA YAAMSHWA, SIMBA YAPATA PIGO** UK.24

**KABWELA** UK. 18

## HABARI KITAIFA




Rais Samia Suhuhu Hassan, akikata utepe kuzindua Maabara ya Sayansi katika Skuli ya Sekondari ya Kizimkazi yenye thamani ya Sh. Milioni 50 iliyojengwa kwa msaada wa Benki ya CRDB, Zanzibar jana. Wengine ni Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Lela Mohammed Musa (wa pili kushoto), Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela (wa tatu kulia), Waziri wa Utumishi na Utawala Bora Zanzibar, Haroun Ali Suleiman (kulia), Naibu Katibu Mkuu wa CCM Zanzibar, Dk. Abdalla Juma Sadala (wa pili kulia) na Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Rashid Hadid Rashid. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Tozo za benki, simu zamwibua Kitwanga

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa zamani wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Charles Kitwanga, ameibuka na kuzungumzia sakata la tozo za benki na miamala ya simu, akikosoa njia zinazotumika katika utozaji wake.

Kitwanga, aliyekuwa Mbunge wa Misungwi kabla ya kuangushwa ndani ya chama katika mchakato wa Uchaguzi Mkuu wa 2020, alikosoa kuhusu tozo hizo jana jijini Dar es Salaam alipozungumza na waandishi wa habari.

Mfanyakazi huyo wa zamani wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT), alimshauri Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, kuachana na masula ya tozo hizo zilizoibua malalamiko na ukosoaji mwingi.

"Jana (juzi), nilimsikiliza kwa makini sana Waziri wetu wa Fedha (Dk. Mwigulu). Tukienda kwenye msingi wa hili, tukianza na walivyoisema wananchi wengi washiriki kuchangia, hapa hayuko sahihi.

"Ukianzia kwenye masuala ya kutuma fedha kwenye mitandao, M-Pesa, Tigo Pesa, Airtel Money na kadhalika, wenye uwezo wa kufanya hivyo tayari ni walipakodi.

"Kwa maana kama mtu anatuma fedha, atakuwa anamtumia ndugu yake, mzazi, ni mfanyakazi au ni mfanyabiashara ambaye ni mkubwa ambaye huwa analipa kodi, lakini mtu wa kawaida kijijini ambaye hana kazi, hawezi kumtumia mtu hivi hivi.

"Tuelewe kwamba wanaoweka (fedha) benki ambako na kwenye fedha zinatozwa tozo ni watu wenye uwezo. Mfanyabiashara, mfanyakazi anaweka fedha benki na huyu anafanya hivyo kwa sababu serikali inamlipa kupitia benki, kwa hiyo analazimika kufungua akaunti.

"Kwa hiyo, fedha zake zinapotoka kwenye mshahara, zinaingia kwenye akaunti yake. Na hata akizichukua zote, bado atatozwa tozo. Lakini hawa tayari fedha zao zimeshatozwa kodi. Sasa unapokuja unazitoza tena tozo, wanaita 'double taxation' (kulipisha kodi mara mbili), ni uvunjaji wa sheria," alifafanua.

Kitwanda, alisema kauli ya Waziri Mwigulu kwamba kutoza tozo hizo ni kupanua wigo wa watu kulipa kodi, haina uhalisia.

"Sasa tunaposema tunapanua wigo wa watu, hatuko sahihi. Tuangalie kwamba ile 'base' (chimbuko) ya walipakodi ambao wana namba ya TIN (namba ya mlipakodi) ni wangapi.

"Logic ya waziri au mafikirio yake ya jinsi ya kuangalia ni mbaya, kwa sababu sasa una tozo kwenye ATM, kwenye akaunti yako unapochukua fedha, kwenye M-Pesa, Tigo Pesa, Airtel Money na kwingineko, yaani kila transaction (mwamala), unayofanya inapigwa kodi, ina maana sasa transactions (miamala) zako za kibenki zinakuwa ghali.

"Badala ya kupunguza ili kupanua hiyo tunayoita financial inclusion, sisi tunakimbiza tunaifinya hiyo, sasa sijui ni uchumi wa wapi huo!" Kitwanga alisema.

Kitwanga, alishauri kuachana na tozo hizo zote na kutafuta njia nyingine za mapato, akitamka: "Mimi ushauri wangu tuachane na hizi tozo zote, tukae na hawa watu wa mitandao ya simu, halafu tuwaulize wanatoza kiasi gani kwa dakika, tuongeze Sh. 60 tu kwenye kila dakika mtu anayopiga, ina maana utakuwa na walipakodi milioni 29, tuwaze kipana, tuwaze mbali, tusiwatese wale wanaolipa kodi.

"Sasa hivi huwezi kuniambia kila mtu analipa kodi, eti umepanua wigo, wigo uko wapi? Anayetuma fedha ni huyo huyo, amezitoa benki ni huyo huyo na anayelipwa mshahara huo huo," alifafanua na kumkaribisha Waziri Mwigulu kumpa ushauri zaidi wa kiuchumi.

"Ninawashauri waje hapa nitawaeleza, nitawapa 'facts, I have data' (ninazo takwimu). Sizungumzi kwa kubahatisha. Kwa mfano, Waziri Mkuu wa kwanza wa Singapole, alikuwa anazungumzia namna walivyoinua uchumi wao, nao walikuwa kama sisi, lakini wako katika top ten (kumi bora) kiuchumi duniani. Tuwaze kwa upana, nchi yetu hii ina watu wengi wenye uwezo sana wa kufikiri, serikali iwatumie, siyo lazima mimi.

"Mimi nimefanya kazi Benki Kuu ya Tanzania miaka 23, kuna PhD nyingi tu. Ni vizuri tukawaza kwamba nchi yetu inahitaji kuendelea, hatuwezi kutegemea tozo, maliasili tulizonazo nyingi namna hiyo, haiwezekani aise!

"Kuna vyanzo vingi mno vya mapato ambavyo hatutaki kuhangaika, tunakwenda kutafuta njia rahisi kupata kodi au tozo . Lakini tunapokwenda huko kwenye njia rahisi, we are killing our economy (tunauua uchumi wetu).

"Transaction na financial transaction ni base ya shughuli ya biashara, sasa kama unaishindilia 'tax' (kodi) itakuwaje? Ile ndiyo inayosababisha biashara ifanyike na biashara ikifanyika ndipo unatakiwa utoze tozo na kodi, sasa wewe unatoza kwenye chanzo, biashara itapatikanaje?

"Acha huku usitoze, 'stimulate' kuwe na 'big financial' na 'transactions' nyingi ambazo zitasaidia watu wazalishe na wakizalisha, toza huko, kwenye matokeo badala ya kutoza kwenye matokeo, unatoza kwenye chanzo cha kusababisha matokeo, mimi sijui tunakwenda wapi, lazima Watanzania sasa tuseme.

"Na mimi nimeamua kusema leo (jana) kwa sababu juzi niliposikia Waziri Mwigulu, atazungumza nilitarajia atazungumza namna ya kuondoa hii, ana alternative (mbadala), badala yake anazungumza kutetea, 'transactions' (miamala) za pesa ndizo zinasababisha watu washughulike kuzalisha, sasa unaziua, fedha zitafikaje?" alihoji.

Kitwanga, alikumbusha kuwa sheria ya kodi hairuhusu kutozwa kodi mara mbili, lakini anachokiona sasa kuna utozaji wa aina hiyo, jambo ambalo siku chache zilizopita, Mwenyekiti wa CHADEMA, Freeman Mbowe, pia alilipinga vikali.

Juzi, akizungumza na waandishi wa habari jijini Dodoma kuhusu tozo hizo, Waziri wa Fedha na Mipango, (Dk. Mwigulu), alisema serikali imechukua maoni yote ambayo yametolewa na wananchi kuhusu suala hilo na itayafanyia kazi na hivi karibuni itatoa tamko kuhusu utekelezaji wake.

Waziri huyo pia alisisitiza kuwa uamuzi wa kuweka tozo hizo ulifanyika kwa kushauriana na wananchi.

# Abiria wakaa saa 3 baharini upepo ukiipiga MV Magogoni

**Na Romana Mallya**

ABIRIA wanaotumia kivuko cha MV Magogoni, jana walikaa saa tatu baharini baada ya kushindwa kushusha watu kutokana na kushindwa kutia nanga.

Hatua hiyo ilisababisha taharuki wakati kivuko hicho kikitokea Kigamboni kwenda kwenye gati ili kushusha abiria, hivyo kushindwa na kupelekwa na upepo mita chache kutoka eneo la kushushia na kukwama ufukweni.

Tukio hilo lilitokea jana majira ya saa 5:30 asubuhi na kusababisha abiria kukwama ndani ya kivuko hicho takribani saa tatu ndipo uokoaji ulipofanyika kupitia kivuko kidogo cha Seataxi mali ya kampuni ya Azam Marine.

Kabla ya hatua ya kuwaondoa watu ndani ya kivuko hazijafanyika, boti ndogo ilifika eneo hilo na kuanza kuivuta kwa kamba lakini haikuwezekana ndipo wakaamua kutumia kivuko kidogo.

Wakizungumza na Nipashe, baadhi ya waathirika walisema hilo ni tukio la pili kutokea likitanguliwa na lingine juzi jioni.

Abdul-Rafik Hassan, mmoja wa abiria waliokumbwa na mkasa huo, alisema tukio hilo lilitokea saa 5:30 asubuhi na kwamba hali hiyo imempa hofu ya kupanda vivuko hivyo kwa sababu anaona si salama.

"Ninaishi Kigamboni na shughuli zangu ninazifanya Posta kwa hiyo kivuko ni usafiri wangu, hata jana (juzi) jioni wakati ninarudi Kigamboni na kivuko hiki, tulipofika katikati kilizima na nahodha alilazimika kurudi hapa na tukachukulia na kivuko kingine," alisimulia.

Abiria mwingine, Levis Mwenewanda, aliishauri serikali iwe na kitengo cha dharura kwa sababu kwa muda ambao wametumia ndani ya kivuko hadi kukolewa imechukua muda mrefu.

"Kivuko kimenasa kwenye mchanga lakini hata watu wanaokuja kuokoa ili kukinasua hawana vifaa vya kuisaidia. Kilichotokea kivuko kinaonekana ni kibovu kwa sababu kilikuwa kinashindwa kuingia kwenye gati.

"Tumetokea Kigamboni kuja Kivukoni, kwanza kinatembea taratibu sana na watu ambao hawajazoea walianza kupata wasiwasi. Tulivyokaribia kwenye gati nahodha wakati anajitahidi kuipeleka pale (gati) ikamshinda ndiyo tukaanza kupelekwa na upepo mpaka kule ufukweni ikaguta pale," alisema.

Mwenewanda alisema amelazimika kuacha gari kwenye kivuko mpaka hapo kitakaponasuliwa na kupelekwa kwenye gati.

Naye Khadija Musa alisema baada ya kivuko hicho kupata tatizo hilo kimesababisha usumbufu kwao kwa sababu wamelazimika kutumia muda mrefu kuvuka.

"Vivuko vinavyofanya kazi ni viliwi na MV. Magogoni ni kivuko kikubwa ikilinganishwa MV.Kigamboni, yaani nimechukua saa zima kuvuka kwa sababu abiria upande wa Kigamboni na huku Kivukoni ni wengi.

"Kivuko cha MV. Kigamboni kibebe magari bado watu na mizigo yake kwa kweli serikali iangalie uwezekano wa kutuletea usafiri salama, MV. Magogoni hii siyo mara ya kwanza kuharibika, wasisubiri tufe ndiyo wanunue vivuko vyenye usalama kwetu," alisema.

Taraifa ya Wakala wa Ufundi na Umeme (TAMESA) iliyotolewa baada ya tukio hilo, ilisema jana majira ya saa sita mchana kivuko cha MV. Magogoni kilipatwa na dhoruba ya upepo mkali na kusukumwa pembezoni mwa gati.

Taarifa hiyo ilisema juhudi za kukinasua zilifanyika na kufanikiwa na kimerejeshwa kwenye gati na kwamba kinafanyiwa ukaguzi kabla ya kuendelea kutoa huduma.

"Wakala unawaomba radhi abiria wote walitumia kivuko cha Magogoni Kigamboni kwa usumbufu uliojitokeza," ilisema taarifa hiyo.




Kazi ya ujenzi wa majengo ya mradi wa stendi mpya ya mabasi Mwenge, ikiendelea katika Manispaa ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam jana, baada ya ujenzi wake kusimama kwa muda mrefu. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# DC aanika madudu ya kutisha serikalini

**Na Beatrice Shayo**, KIGOMA

MKUU wa Wilaya ya Kigoma, Ester Mahawe, amesema kuna madudu ya kutisha serikalini, hivyo kushauri mkurugenzi wa halmashauri anapotumbuliwa, wakuu wa idara na vitengo pia wahusishwe kwa kuwa wanashiriki katika kukwamisha ufanisi wa kazi.

Pia ameshauri kufanyika kwa mabadiliko ya sheria kwa watumishi wa serikali kwa kupewa mikataba ya muda wa ajira ili waache kufanya kazi kwa mazoea. Mahawe aliyasema hayo juzi wakati Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, Kanali Mstaafu Abdulrahman Kinana, akiwataka viongozi kujibu kero zilizowasilishwa na wananchi.

Mahawe alisema awali alikuwa anafanya kazi sekta binafsi kabla ya kuteuliwa na kuweka bayana kwamba kama kweli wanataka kuijenga Tanzania ya watu waadilifu na wachapa kazi, ifike wakati kubadilishwe sheria za ajira.

"Zisiwe hizi za 'permanent and pensionable' (ajira za mkataba wa kudumu). Sheria hii inawaumiza wateuliwa wa Rais hasa wakuu wa wilaya, wakuu wa mikoa na wakurugenzi. Watu ambao hawatekelezi majukumu yao katika Halmashauri ni wakuu wa idara," alisema.

Kwa mujibu wa Mahawe, watu hao hawatekelezi majukumu yao kwa sababu wanajua mkurugenzi atatumbuliwa na mkuu wa idara ya elimu, afya na mhandisi wa majengo wao watabaki.

"Ninaomba ifike mahali Mkurugenzi anavyotumbuliwa aondolewe na wakuu wa idara wote kwa sababu tunawaumiza watu wasio na hatia. Mkurugenzi ni mtu mmoja, chini yake ana wakuu wa idara 14. Wakiamua kumkwamisha, gurudumu haliendi. Watu hawa wanafanya kazi kwa mazoea kwa sababu wanajua hawawezi kuondolewa. Tufanye tu kama sekta binafsi mtu anaajiriwa kwa mkataba maalum," alisema.

"Utakuta mtumishi ameajiriwa akiwa na miaka 25, anasubiria kufa au kustaafu. Watu wa namna hiyo wamekuwa wakwamishaji wakubwa wa maendeleo," aliongeza.

"Hapa kwetu kwa mfano, tumepata changamoto ya wizi wa dawa kwenye halmashauri yangu. Zahanati 10 zimeibiwa dawa ambazo zinafanana na zinauzwa mtaa wa pili watu wapo na wanaendelea kula mshahara.

"Makamu Mwenyekiti bunge lipo na mimi nilishapita bungeni. Bunge lipo kwa ajili ya kubadilisha sheria. Tusiendelee kuishi kwa mazoea. Kama kweli tumepanga kumsaidia Rais, tubadilishe sheria badala ya watu kusubiri kustaafu , basi wafanye kwa mikataba,' alisema.

**MADUDU BANDARI**

Mkuu huyo wa wilaya alisema kero zilizoko bandarini ni nyingi kutokana na kuwapo kwa tozo nyingi na kusababisha kukosekana kwa mapato.

"Nikiangalia fedha inayopotea hapa na Rais anaenda nje kutafuta fedha, ninaumia sana. Ushauri wangu hizi taasisi kubwa mfano TRC (Shirika la Reli Tanzania), TPA (Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania na TRA (Mamlaka ya Mapato Tanzania) ifike mahali wawekwe watu ambao wana uzoefu wa biashara.

"Serikali inapata hasara na mtu hajali ilimradi anakula ana gari lina kiyoyozi maisha yake yanaendelea na watoto wanasoma Ulaya. Kwa namna hii hatutatoboa," alisema.

Alisema kuna mambo ambayo yako ndani ya uwezo na anapoteuliwa hajawekwa hapo kama sofa. Kazi yake ni kuishauri serikali jambo gani la kufanya na kama kuna kikwazo anaeleza ili mambo yaende.

Alisema jambo jingine linalokera ni wakala wa serikali wanaohusika kufanya maisha ya wananchi kuwa magumu.

"Huwezi kuamini maji ya kunywa au juisi yenye ithibati ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kama vinavuka kwenda Congo ni lazima watu wa mionzi wachukue kwenda kupima kabla ya kuruhusiwa.

Pia alisema ana mwaka mmoja na miezi miwili tangu alipofika Kigoma na katika majukumu yake mengi anayoyafanya ni kusuluhisha kesi za ardhi.

# Bunge lanusa harufu ufisadi wa mabilioni

**Na Augusta Njoji**, DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), imetoa miezi mitatu kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kufanya ukaguzi maalum wa mkopo wa Sh. bilioni 20 ambao Manispaa ya Moshi iliingia mkataba na Benki ya Uwekezaji (TIB) kwa ajili ya ujenzi wa stendi ya kimataifa.

Akitoa maazimio ya kamati hiyo baada ya kuchambua hoja za ukaguzi za manispaa hiyo jana, Makamu Mwenyekiti wa LAAC, Selemani Zedi, alisema stendi hiyo inajengwa kwenye Kata ya Mfumuni na ukaguzi huo umeagizwa kutokana na kuwapo na mkanganyiko.

"Baada ya mahojiano kati yetu na Halmashauri ya Manispaa ya Moshi, tumemwagiza CAG kwenda kufanya ukaguzi maalum kuhusu mkopo wa Sh. bilioni 20 ambao Manispaa ya Moshi iliingia mkataba na TIB kwa ajili ya ujenzi wa stendi hiyo," alisema.

Makamu Mwenyekiti huyo alisema kwenye maelezo yaliyotolewa na viongozi wa manispaa hiyo, halmashauri hiyo iliingia mkataba na TIB kukopa fedha hizo kwa ajili ya kujenga stendi hiyo.

"Baadaye walituambia kwamba walipata barua ya zuio kutoka TAMISEMI walisipate mkopo huo lakini wakati huo huo, mkopo huo ndani yake kulikuwa na Sh. milioni 378 ambazo zilikuwa ni malipo ya Mhandisi Mshauri.

"Sasa wao wanatuambia wamezuiwa wasiendelee na mkopo lakini wakati huo huo wanasema zile Sh. milioni 378 za Mhandisi Mshauri zilitoka, yaani TIB ilitoa fedha hizo kumlipa huyo mhandisi anayeitwa Digital Space Consultancy,"alisema.

Alifafanua kuwa mhandisi huyo alilipwa fedha hizo wakati ni sehemu ya mkopo wa Sh. bilioni 20, ambao manispaa imeeleza TAMISEMI ilizuia wasipate mkopo huo.

"Tunataka tujue kama mkopo ulizuiwa, iweje Kampuni ya Digital Space Consultancy ikalipwa fedha hizo, Sh. milioni 378 kwa ajili ya kutoa huduma ya ushauri wa mradi huo? Mazingira haya yamesababisha kamati iagize," alisema.

Hata hivyo, alisema sababu zilizoelezwa kwa kamati na manispaa hiyo ni kwamba mkopo huo ulizuiwa kwa halmashauri zote nchini kuchukua mikopo kwa benki za kibiashara na kuwataka waandike maandiko wawasilishe Hazina ili iwatafute fedha za kutekeleza miradi hiyo.

"Kwa hiyo, wamesema sababu za kutoendelea na mikopo hiyo ni kutokana na agizo lililotoka la kuzuia halmashauri kuchukua mikopo kutoka benki za kibiashara, wanasema wakati agizo hilo linatolewa wao mkataba ulikuwa umeanza kutekelezwa ndiyo maana Sh. milioni 378 ikatoka," alisema.

Aliongeza kuwa, kamati inaona kama fedha hiyo ilitolewa, inawezekana mkopo huo ulikuwa umetoka.

Alipoulizwa kuhusu uendelevu wa ujenzi wa mradi huo, Makamu Mwenyekiti huyo alisema pamoja na mradi kuhitaji Sh. bilioni 20, Hazina walikubali kuwapatia Sh. bilioni saba na hadi sasa Sh. bilioni mbili zimetolewa.

# TMA yatabiri upungufu wa mvua za vuli

**Na Faustine Feliciane**

MAMLAKA ya Hali ya Hewa Tanzania (TMA) imetabiri kuwapo upungufu mkubwa wa mvua za vuli katika mikoa inayopata mvua mara mbili kwa mwaka pamoja na ongezeko la hali ya joto kuliko kawaida.

Akizungumza jana wakati akitoa utabiri huo, Mkurugenzi Mkuu wa TMA, Dk Agnes Kijazi, alisema mifumo ya hali ya hewa inaonyesha kuwepo na hali hiyo itakayoleta athari mbalimbali.

"Tunatarajia katika kipindi hiki kuwapo kwa upungufu wa unyevunyevu kwenye udongo katika maeneo mengi yanayopata mvua mara mbili, hivyo kuathiri sekta ya kilimo. Lakini pia tunatarajia upungufu wa maji safi na salama, hivyo kuchochea magonjwa ya mlipuko," alisema Dk. Kijazi.

Alisema upungufu wa malisho na maji kwa mifugo unaweza kusababisha migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi.

"Wananchi na wataalam katika sekta mbalimbali tunawashauri kuchukua hatua kukabiliana na upungufu huu wa mvua. Maofisa ugani wawashauri wakulima kupanda mazao yanayostawi kwenye mvua ndogo, mazao kama miogo, viazi vitamu, mtama na mazao jamii ya kunde," alisema.

Pia alisema kwa sekta ya mifugo, wananchi wanashauriwa kuweka mikakati ya kuhifadhi maji na malisho ya mifugo pamoja na kujiandaa kukabiliana na wadudu kama kupe na wengine warukao.

Aliitaja mikoa itakayoathirika na upungufu huo wa mvua kuwa ni pamoja na Kanda ya Kaskazini husustan Arusha, Manyara na Kilimanjaro. Pia hali hiyo itaikumba mikoa ya Pwani, Dar es Salaam, Tanga, Zanzibar na maeneo ya kaskazini mwa Morogoro.

"Lakini pia upungufu huu wa mvua utatokea kwenye mikoa ya Kanda ya Ziwa, Mwanza, Geita, Kagera, Shinyanga, Simiyu, Mara, kaskazini mwa mkoa wa Kigoma (wilaya za Kibondo na Kakonko).

"Kutokana na mifumo kuonyesha upungufu huu wa mvua, tunatarajia kuongezeka kwa hali ya joto kwa mikoa tajwa," alisema Dk Kijazi na kubainisha kwamba mvua zitachelewa kuanza kunyesha katika maeneo mengi, hivyo kusababisha kuchelewa kumalizika.

Mvua hizo, alisema zitaanza kunyesha kuanzia wiki ya nne ya Septemba katika mikoa ya Kanda ya Ziwa na wiki ya tatu na ya nne kwa mikoa mingine na msimu wa mvua hizo utakwenda mpaka Januari, mwakani.

"Pamoja na upungufu huu wa mvua, tunatarajia kuwepo kwa vipindi vifupi vya mvua kubwa kwa baadhi ya mikoa," alisema.

Dk. Kijazi aliwashauri wananchi pia waendelee kufuatilia taarifa za hali ya hewa wanazozitoa kupitia vyombo vya habari.

# Mkemia anoa viziwi matumizi ya kemikali

**Na Mary Geofrey**

MAABARA ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) imetoa mafunzo kwa kundi la viziwi kuhusu majukumu ya mamlaka na namna ya kujikinga na matumizi ya kemikali katika shughuli zao za kila siku.

Mkemia Mkuu wa Serikali Dk. Fidelice Mafumiko, alifungua mafunzo hayo jana jijini Dar es Salaam na kulitaka kundi hilo kuchukua tahadhari dhidi ya matumizi yasiyo sahihi ya kemikali ambayo yameshasababisha ulemavu kwa wengine.

"Nimeambiwa miongoni mwenu wapo waliopata ulemavu kutokana na kemikali walizotumia sehemu mbalimbali walikokuwa wakifanya kazi. Hata hivyo, sote tunajua umuhimu wa kemikali katika maisha ya kila siku ya mwanadamu," alisema.

Dk. Mafumiko aliwaeleza washiriki hao kemikali zinatumika katika sekta mbalimbali ikiwamo sekta ya afya na malighafi zinazotumika katika kutengeneza dawa au vitendanishi.

Alibainisha kuwa baadhi ya dawa za mifugo na kilimo hutengenezwa kwa kutumia kemikali, hata sekta ya madini hutumia kemikali katika uchimbaji na uchenjuaji wa madini kama vile madini ya dhahabu.

Alisema kemikali pia hutumika kuua vijidudu wakati wa kusafisha, kutakatisha maji.

"Kwenye viwanda vyetu kemikali hutumika katika uzalishaji wa bidhaa mbalimbali kama vile, nguo, pombe kali, rangi za nyumba, magodoro na vyakula vya aina mbalimbali.

"Hivyo basi, pamoja na mada mbalimbali mtakazofundishwa leo (jana), ndani yake mtafundishwa matumizi salama ya kemikali ili kuwa na uelewa wa pamoja na kutumia kemikali hizo bila kuleta madhara. Kwa kufanya hivyo amlaka itakuwa imetimiza jukumu lake la msingi la kulinda afya ya jamii na mazingira," alisema.

Dk. Mafumiko alisema mafunzo hayo yaliyohusisha washiriki 65, yanalenga wapate uelewa mkubwa kuhusu majukumu yanayotekelezwa na mamlaka hiyo na kuwa mabalozi wazuri wa kueneza elimu hiyo kwa jamii, wakiwamo wanachama wenzao, ndugu, jamaa na marafiki.

Aliahidi mamlaka hiyo itaendelea kuelimisha makundi ya watu wenye ulemavu kupitia vikundi vyao ili kuhakikisha wengi wao, kama siyo wote, wanapata uelewa.

# Kigogo atoa angalizo fukuzafukuza ya polisi

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

NAIBU Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini wa zamani, Balozi Dk. Omari Abdurahaman Kaniki, ameacha ujumbe mzito kwa Jeshi la Polisi, akitaka busara itumike wakati wa matumizi ya kanuni zinazoliongoza Jeshi hilo (PGO), vinginevyo fukuzafukuza itaumiza askari wengi.

Balozi Dk. Kaniki, ambaye pia amestaafu akiwa Mkuu wa Chuo cha Diplomasia nchini, aliacha ujumbe huo jana akiwa Shule ya Polisi Moshi (TPS), alipokwenda kuagwa rasmi baada ya kustaafu.

Katika hafla hiyo, Kaniki aliagwa na Mkuu wa Jeshi hilo, IGP Camilius Wambura na makamishna wa polisi.

Akizungumza baada ya kuagwa, Balozi Dk. Kaniki alisema: "Kwa mfano, sisi Jeshi la Polisi tuna taratibu ambazo ziko wazi, kuna PGO (Kanuni Zinazoliongoza Jeshi la Polisi) na sheria mbalimbali.

"Hivyo, haina budi sheria, taratibu na kanuni hizi zinazoongoza jeshi zitumike lakini kwa busara kubwa bila kufanya hivyo, unaweza ukatoa adhabu ambayo ni kubwa kulingana na kosa lililotendeka."

Kuhusu matumizi hayo ya busara kabla ya kutoa adhabu, alisema: "Ninasisitiza kila mmoja wetu pale alipo atekeleze majukumu yake kwa mujibu wa sheria, kanuni, taratibu na mila zetu ambazo tumejiwekea lakini cha muhimu zaidi ni huruma, pale ambapo huruma inapohitaji kutumika, basi itumike kwa sababu hakuna mkamilifu asilimia 100, sisi sote ni binadamu, kuna kuteleza kwa namna moja au nyingine.

"Cha muhimu ni kuangalia kuteleza huko kumeathiri vipi taasisi anayoiongoza kama ni mambo yanayovumilika, basi aonywe na aambiwe ajirekebishe na maisha yaendelee kwa sababu ukisema kila anayefanya kosa utamfukuza, utabaki na nani lakini haina maana kwamba waangalıwe tu, hapana! Tuchukue hatua stahiki kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa."

Balozi Dk. Kaniki pia aliwaachia ujumbe askari, akitamka: "Ujumbe ninaouacha ni uaminifu na uadilifu hasa katika nafasi kubwa kama hizi ambazo tumependelewa.

"Cha msingi ni kuwa wasemaji kwa wasio na wasemaji kwenye zile nafasi mbalimbali wale ambao wamefanikiwa kuzishika, hebu waangalie wale wanaowaongoza katika nafasi mbalimbali kwamba wana matatizo gani na ni jinsi gani ya kutambua matatizo yao.

"Je, wanapata fursa na wao wenyewe kuendelea maana hakuna anayezaliwa akiwa ni kiongozi, suala la maendeleo tu ya kitaaluma yanayomfanya mtu kufikia katika ngazi mbalimbali.

"Waliobaki wasiwe wachoyo katika nafasi ya kuwaendeleza wale walio chini yao ili siku zinazofuata nao washike, ukiwaficha kuna miaka inafika una miaka 60 sasa wale unawachaje, ofisi unaiachaje?"



Vijana wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wakiwa wamebeba jeneza lenye mwili wa aliyekuwa Mwanahabari mkongwe nchini, marehemu Charles George Kizigha, wakiutoa nyumbani kwake Africana, kwa ajili ya kuupeleka Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Usharika wa Mbezi Beach, kwa ibada na baadaye mazishi yake kufanyika kwenye makaburi ya Kondo Ununio, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# PIC yabaini tatizo katika mtaji wa TADB

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma (PIC) imeagiza serikali kufanya jitihada za makusudi za kuongeza mtaji kwenye Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) ili mapinduzi ya kilimo yaliyofanyika kwenye bajeti ya kilimo yawe na tija nchini.

Mwenyekiti wa kamati hiyo, Jerry Silaa, alitoa agizo hilo la kamati jana jijini hapa baada ya kuhoji viongozi wa benki hiyo.

Alisema kamati imeona nia ya dhati ya Rais Samia Suluhu Hassan kuweka nguvu kubwa na kuboresha sekta ya kilimo ambayo inaajiri Watanzania asilimia 69.1.

"Bajeti ya mwaka huu imekua mara nne, tumekuwa na bajeti ya kilimo kubwa, lakini pia bajeti ya mifugo na uvuvi imekua, hivyo kamati imeona jambo moja unapokuza bajeti ya kilimo, kamati inaona kuwe na nia ya dhati wakati inakuza bajeti ya kilimo, lazima ikuze na mtaji wa Benki ya Kilimo," alisema.

Silaa alisema kamati imeona itie nguvu kwenye hilo kwa kukaa na serikali ifanye jitihada za makusudi za kuongeza mtaji kwenye benki hiyo.

"Mtaji ukiongezeka unaposikia bei ya unga imepanda, mafuta imepanda, ukali wa bei za vyakula maana yake uzalishaji wa kilimo upo chini. Ukiwezesha hii benki maana yake kilimo kitaboreka na mazao yatazalishwa kwa wingi na kutakuwa na usalama wa chakula na kushusha bei, tutazalisha mafuta ya kula na kupunguza utegemezi wa kuagiza.

"Ongezeko la mtaji kulinganishwa na mwaka 2020 ilikuwa na mtaji wa Sh. bilioni 76.7 na mwaka 2021 mtaji ulifikia Sh. bilioni 295.6, na madeni yalipungua ambapo mwaka 2019 madeni yalikuwa Sh. bilioni 260, mwaka 2020 madeni yalikuwa Sh. bilioni 300 na mwaka 2021 yalishuka hadi Sh. bilioni 67," alisema.

Alisema serikali ilifanya maboresho mtaji kupitia mkopo wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB) wa Sh. bilioni 208, ambapo iligeuza mkopo na kuwa mtaji.

Pia alisema PIC imeridhishwa na utendaji wa benki hiyo kutokana na kufanya vizuri mwaka hadi mwaka ambapo kwa mwaka 2019 ilipata faida ya Sh. bilioni 3.06, mwaka 2020 ilipata Sh. bilioni 8.22 na mwaka 2021 ilipata Sh. bilioni 10.9.

Alisema kuwa Agosti mwaka jana kamati ilikutana na benki hiyo ambayo serikali inamiliki hisa kwa asilimia 100 na kutoa maagizo manne ambayo imepokea utekelezaji wake.

Mwenyekiti wa Bodi ya Benki hiyo, Ishmael Kasakwa, alisema bodi itahakikisha inasimamia utekelezaji na ushauri wa kamati kwa benki hiyo ili kuwa na kilimo chenye tija.

Mkurugenzi wa Benki hiyo, Frank Nyabundege, alisema tangu kuanzishwa kwake, benki hiyo imetoa mikopo ya Sh. bilioni 429.5.

PIC inafanyia kazi hoja zilizoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu benki hiyo zilizomo katika ripoti yake ya ukaguzi wa mashirika ya umma kwa mwaka 2020/21 iliyowasilishwa bungeni Aprili 12 mwaka huu.

Air Tanzania
The Wings of Kilimanjaro

# EXCITING CAREER OPPORTUNITY

Air Tanzania Company Limited (ATCL) is expanding its network to meet the needs of its Business Strategy which focus on sustaining the recorded achievements and remain an airline of choice that meets and exceeds customers' expectations in line of its mission of provision of reliable, safe, and high-quality services. Therefore, applications are invited from qualified Tanzanians to fill the positions mentioned below;

**1. POSITION: FLIGHT PURSER (Senior Cabin II) - (15 POST)**

**1.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS AND WORKING EXPERIENCE:**

- Must have a minimum of Form IV Certificate with Four Credit passes of which ONE of them should be English and;
- Must hold Ab-Initio Certificate from Recognized Aviation Institution plus Cabin Crew License from Tanzania Civil Aviation Authority (TCAA);
- Must have working experience of at least seven (7) in related field, of which (3) years must be minimum flying experience as Senior Cabin Crew.
- Must have attended Forward Galley Course and Leadership training
- Must be Fluent in both written and spoken English and Swahili
- Height from 5.0 feet, acceptable Level of BMI
- Must have no visible tattoos while in Air Tanzania crew uniform
- Knowledge of extra international language will be an added advantage
- Diploma and knowledge of additional international language is an added advantage

**1.2. DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

- Direct, co-ordinate, organize and supervise the functions and tasks of the cabin crew by making sure the customers receive the best possible service and ensure all standards and expectations are met.
- Prepare and carry out pre-flight briefing and post-flight debriefing.
- Assign duties and delegate particular responsibilities relating to passengers requiring special attention/ care.
- Observe and assess individual crew performance, discuss with the crewmember, offer support where necessary and provide reports to the Chief Cabin Crew/Stewardess with recommendations as and when required.
- Be responsible to the PIC for the management of safety and security outcomes of cabin and emergency procedures specified in the General Operations Manual, and for their observance for the conduct and management of cabin safety by the cabin crew and by all passengers.
- Inform the PIC of all irregularities and malfunctions and, at the prescribed times, report cabin sterile.
- Ensure that cabin operations are conducted in accordance with the applicable regulations and standards of the organization.
- Report to the Captain and/ or duty engineer of all unserviceable items.
- Liaise with station manager/ PAS representative, at lay over station, in matters related to cabin crew.
- Ensure that out station rules and regulations are adhered to.
- Ensure proper utilization and handover of in-flight catering items, materials and good care of in-flight equipment.
- Develop crewmembers to be able to perform all duties on a flight by carrying out on the job training/ coaching for newly promoted and recruited cabin crew.
- Ensure that, at the end of a flight, all documentations, logs and reports are completed.
- Conduct Competency checks for cabin crew.
- Set an example for cabin crew and provide counselling as required; be self-disciplined, adhere to all company rules and regulations so as to be able to instill discipline.
- Collect feedbacks from the crew and passengers and make suggestions and recommendations for improvement to be made on
- Perform any other official duties as may be assigned by a supervisor.

**2. POSITION: CABIN CREW II (34 POSTS)**

**2.1. MINIMUM ENTRY QUALIFICATIONS AND WORKING EXPERIENCE**

- Must have a minimum of Form IV Certificate with Four Credit passes of whichONE of them should be English and;
- Must hold Ab-Initio Certificate from Recognized Aviation Institution plus Cabin Crew License from Tanzania Civil Aviation Authority (TCAA);
- Must have a valid class 2 medical certificate acceptable to the Authority
- Must be Fluent in both written and spoken English and Swahili
- Must have no visible tattoos while in Air Tanzania crew uniform
- Height from 5.0 feet, acceptable Level of BMI
- Knowledge of Extra International Language will be an added advantage

**2.2.DUTIES AND RESPONSIBILITIES**

- Ensure passengers safety and security from the time passengers aboard the aircraft until the time they disembark.
- Inform passengers on emergency, safety and security procedures during all phases of the flight and manage procedures following an emergency in accordance with this manual and the PIC instructions.
- Ensure cabin safety and security under the overall authority and responsibility of the PIC (i.e the safety of passengers and security of cabin load and galleys)
- Responsible to read and sign all notices or bulletins as required.
- Attend preflight and post flight briefing as required
- After boarding the aircraft cabin crew shall carry out a cabin security check, verify the safety emergency equipment, catering equipment's and immediately report any deficiencies to the Flight Purser/ In charge cabin crew for further action.
- Ensure passengers respect and comply with the "fasten seatbelt" and "No smoking "signs and other safety and security instructions while in flight.
- Ensure the passengers safely escape in an emergency evacuation.
- Form the liaison between passengers and the flight crew
- Provide optimum comfort and service to the customers.
- Report to the Senior Cabin Crew and Flight Purser any incident that has endangered or may endangered safety of the operations while on flying duties the Cabin crew is required to follow all lawful directions given by the Senior Cabin Crew/Flight Purser (in charge cabin crew)
- Ensures the safety and security of passengers, crew and aircraft through adherence to Company policies and standard operating procedures.
- Deliver world class passenger service and assist in on-time performance
- Perform any other official duties as may be assigned by a supervisor.

**3. TERMS AND CONDITIONS:**

Five (5) years contract with attractive remuneration and fringe benefits as per ATCL Salary Structure and Incentive Scheme.

**4. MODE OF APPLICATION FOR ALL APPLICANTS:**

Interested applicants must submit a dully signed letter for consideration of the application attached with the following:

i. A curriculum vitae (CV),
ii. Certified copies of all certificates (including secondary school, birth certificates), other relevant certificates, Applicants who have studied outside Tanzania should have their certificates approved by relevant authorities Tanzania Commission for University (TCU) or National Examination Council-NECTA)
iii. Two recent passport size photographs
iv. A full size picture dressed in business attire
v. Name and address of at least two reputable referees;
vi. Applicant's reliable contact address, email address and telephone number.

**Note: Misrepresentation of qualifications or any other information on application shall warrant legal consequences**

**5. CLOSING DATES:**

Applicants should reach the undersigned within 14 days from the first date of this announcement.

**MANAGING DIRECTOR & CEO,**
**AIR TANZANIA COMPANY LIMITED,**
**P.O. Box 543,**
**DAR ES SALAAM.**
**Issued on 2nd September, 2022**

217027102

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila la kheri Taifa Stars kuelekea fainali CHAN

**TIMU** ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), inatarajia kushuka dimbani jijini, Kampala leo kuwakabili wenyeji Uganda (The Cranes), katika mechi ya marudiano ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN).

Katika mchezo wa kwanza uliochezwa Jumapili iliyopita kwenye Uwanja wa Benjamini Mkapa, Dar es Salaam na kusimamiwa na waamuzi kutoka Sudan Kusini, Taifa Stars ilifungwa bao 1-0.

Baada ya kumalizika kwa mchezo huo, siku iliyofuata Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), lilitangaza kuachana na aliyekuwa Kocha Mkuu, Kim Poulsen, na mikoba yake kumkabidhi Mzambia, Honour Janza na nahodha wa zamani wa kikosi hicho, Mecky Maxime.

Janza na Maxime waliongoza kikosi hicho juzi na kikubwa walieleza wanakwenda huko kupambana na kuhakikisha wanapata matokeo chanya na hatimaye wanasonga mbele kwenye michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

Nipashe, tunawakumbusha viongozi wa TFF, benchi la ufundi, wachezaji na wadau waamini kazi bado haijamalizika na si kwa Tanzania ambayo iko nyuma, hata kwa Waganda ambao wako mbele kwa goli moja.

Janza na kikosi chake wanatakiwa kufahamu wamekwenda Uganda kupeperusha bendera ya nchi, hivyo kila mmoja anawajibu wa kutimiza majukumu yake kwa kiwango cha juu ili kufikia mafanikio na malengo ambayo yanatarajiwa.

Wachezaji wa Taifa Stars wanatakiwa wasifikirie matokeo ya mechi iliyotangulia na badala yake wajikite kupambana kusaka ushindi katika mchezo ulioko mbele yao kwa kuamini wako katika fainali na matokeo wanayoyahitaji ni ya ushindi tu na si vinginevyo.

Kwa kuweka mawazo katika mchezo huo, itawasaidia kupata nguvu kwa sababu hakuna kisichowezekana, kama Waganda walipata ushindi katika dakika 90 za kwanza, basi inawezekana nao wakapata matokeo chanya kwenye dakika kama hizo zilizobakia.

Kama timu hiyo ikiwa na Juma Kaseja langoni mwaka 2019, Kocha Mrundi, Etienne Ndayiragije, ilifanikiwa kuwachapa Sudan mabao 2-0 wakiwa kwao Khartoum na kufuzu fainali za CHAN, ikumbukwe Stars ilifungwa goli 1-0 hapa nyumbani, pia mwaka huu inawezekana ikarudia rekodi hiyo na kubakia kwenye mashindano.

Kuongeza juhudi na umakini, kufuata maelekezo ya benchi la ufundi na kutokubali wenyeji wamiliki mpira kwa kiasi kikubwa, ni mambo ambayo yataisaidia Stars kuvuka kwenye mtihani ambao uko mbele yao.

Mbali na wachezaji kuipa nchi matokeo chanya, wakumbuke mashindano hayo ni daraja la kutangaza vipaji vyao kwa mawakala mbalimbali wanaofuatilia michuano hiyo ambao wanasaka nyota wa kuwapeleka kwenye klabu mbalimbali za Ulaya.


Sifa ya kwanza ya mchezaji kupata klabu kwenye mataifa ya Ulaya ni kuonekana katika kikosi cha nchi yako, sasa kama mchezaji atakayepata nafasi na akajituma, huyo atakuwa amejiandalia 'tiketi' ya kufuatwa na mawakala na kuwafanya watimize ndoto zao za kucheza soka la kulipwa kwenye mataifa hayo yaliyoendelea.

Mbali na kufikiria kupata timu nje, lakini mechi hizi za mashindano ya CHAN, ni nafasi nyingine muhimu kwa wachezaji ambao walikuwa wanakosa namba kwenye kikosi cha Stars kinachoshiriki mashindano mengine, kulishawishi benchi la ufundi na hatimaye kuingia kwenye 'first eleven' ya Tanzania.

Tunawakumbusha mashabiki na wadau wa soka walioko sehemu mbalimbali kwamba huu ni wakati wa kuungana na timu hiyo kuiombea dua njema ili ifikie malengo na si muda wa kutafuta 'mchawi' huku wapinzani wetu wakiendelea kuungana.

Tunafahamu vyema umoja na ushirikiano huzaa matunda, tunawakumbusha mashabiki ambao watapata nafasi ya kwenda Kampala kuwashangilia, wafanye hivyo kwa sababu itawaongezea nguvu wachezaji wetu na kujiona wanawajibu wa kupambana hadi kwenye tone la mwisho.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






Na Adam Fungamwango

## Muungwana Lazima Nilonge

# Nyota Simba Queens awe kioo kwa wachezaji wakike

**MOJA** kati ya usajili bora kufanywa na Simba Queens msimu huu ni wa kiungo mkabaji kutoka nchini Kenya, Vivian Corazone, ambaye alikuwa akiichezea Gaspo Youth FC.

Si wengi walikuwa wanajua ni mchezaji mzuri, ingawa binafsi nilimwona akiwa na Timu ya Taifa ya Kenya (Harambee Starlets), iliyokuja nchini kushiriki mashindano ya Kombe la Chalenji ya Afrika Mashariki na Kati kwa wanawake yaliyofanyika mwaka 2019 na kufanikiwa kutwaa kombe hilo, mechi ya fainali wakiifunga Twiga Stars mabao 2-0.

Sikuwa na wasiwasi na uwezo wake, ingawa nilidhani angepata tabu kwenye mechi za mwanzo kama kawaida ya baadhi ya wachezaji ambao ni lazima kwanza azoee mazingira.

Kilichotokea ni kwamba hata kabla ya Ligi Kuu ya Wanawake ya Tanzania haijaanza, amefanya vyema kwenye michuano ya Afrika Mashariki na Kati kwa ngazi za klabu Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati (CECAFA).

Alicheza kama vile yupo katika kikosi cha Simba Queens kwa misimu kadhaa. Hata uchangamfu wake ndani na nje ya uwanja ilionekana kama ni mchezaji wa muda mrefu.

Katika michuano ya CECAFA , pamoja na kwamba ni kiungo mkabaji, alifunga mabao matano ambayo kwa kiasi kikubwa yaliiwezesha Simba Queens kutwaa ubingwa na kupata nafasi ya kuuwakilisha ukanda wake kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake itakayofanyika mwezi ujao nchini Morocco.

Kwenye mechi ya fainali dhidi ya She Corporate, pamoja na ugeni yake alichukua jukumu la kupiga mkwaju wa penalti.

Akajitoa muhanga licha ya kwamba kulikuwa na wachezaji wengi wazawa kama Oppa Clement, lakini pia wageni ambao wapo kwenye kikosi kwa muda mrefu kama vile Mrundi Joelle Bukuru.

Akaukwamisha mpira wavuni na lilikuwa bao pekee kwenye mchezo huo lililoifanya Simba Queens kutwaa ubingwa.

Corazone ambaye alianza soka akiwa na miaka tisa tu akiwa Mikongeni High School alikonga nyoyo za mashabiki wa Simba Queens kutokana na umahiri wake kwenye kukaba, akitumia urefu na nguvu alizonazo, akiwa pia na uwezo wa kumiliki mpira, na kupiga pasi ndefu kwa usahihi.

Kwenye vibanda umiza, baadhi ya mashabiki wa Simba, walisikika wakisema wangepata kiungo kama Corazone mwenye uwezo wa kukaba vile na kupiga pasi ndefu kwenda kwa mawinga na mastraika kwa haraka na usahihi kwenye timu ya wanaume, wangefurahi sana.

Baada ya sifa hizi, Corazone ana sifa nyingine ambayo ndiyo ingefaa sana kuwa somo kwa wachezaji wa soka la wanawake Tanzania.

Nalo ni kuendelea kujiweka kama mtoto wa kike.

Pamoja na umahiri wote, kiasi cha kuchaguliwa kuwa mchezaji bora wa michuano, Corazone ni mrembo hasa. Amebaki kuwa mwanamke halisi. Ukimwona nje ya uwanja unaweza kukataa kama ni mcheza soka.

Hii inaondoa dhana ya wachezaji wengi wa soka la wanawake hasa Tanzania kuwa ni lazima wajiweke kama wanaume ndiyo ucheze kandanda.

Labda ukiendelea kuonekana kama mtoto wa kike huwezi kuwa na nguvu na uwezo wa kucheza, hii si kweli.

Corazone amethibitisha msichana anaweza kucheza kwa kiwango cha hali ya juu, lakini akiendelea kubakia na haiba ile ile ya kike.

Wakati soka la wanawake likianza na hata leo hii, baadhi ya wachezaji wamekuwa wakijiweka kama wanaume kuanzia uvaaji, unyoaji, mapozi na hata utembeaji, hii si sahihi, haifai na umefika wakati nyota hao wabadilike.

Hii imewafanya wazazi wengi kukataa au kuwapiga marufuku watoto wao wa kike kujiingiza kwenye soka kwa kuogopa watapotea.

Wanaona kuna maisha baada ya soka, hivyo wakianza kuwa na haiba ya kiume inaweza kuwaletea matatizo mbele ya safari ya maisha yao.

Angalau kwa miaka ya hivi karibuni baadhi ya wachezaji wameanza kujirekebisha, lakini kuna waliodhani wachezaji wanaojiweka kike zaidi wanakuwa na uwezo wa kawaida tu, hawawezi kuwa mastaa zaidi kwa jinsia yao huku wengine wanaojiweka kama wanaume.

Kiungo huyo wa Kenya ameondoa dhana hiyo kwa wachezaji aliokuwa nao, kwani nimeona hata baadhi ya wenzake kwenye timu wameanza kumuiga.

Nadhani hata wachezaji wengine wa klabu za Ligi Kuu ya Wanawake , Corazone anaweza kuwa kioo kwao, kwa kuthibitisha unaweza kucheza soka huku ukiendelea kuwa mrembo.

Amewafanya mpaka baadhi ya wazazi ambao walikuwa wakimshuhudia kwenye televisheni shughuli aliyokuwa akiifanya uwanjani, licha ya urembo wake kulegeza kamba na kuwaruhusu watoto wao wa kike kuingia kwenye soka, lakini wabaki kama Corazone kwa sababu kumbe inawezekana.

# Aachiwa kwa masharti baada ya kukiri kuua bila ya kukusudia

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu, imemuachia kwa masharti ya kutokutenda kosa kwa kipindi cha miaka miwili mshtakiwa Yasir Halfan (21), baada ya kukiri kosa la kuua bila kukusudia.

Halfan alimchoma kisu Chawima Adam shingoni na kufariki dunia baada ya kutokea ugomvi baina yao. Mshtakiwa alikuwa akimdai Adam fedha wakati wakicheza kamali.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi, ambapo alimtia hatiani mshtakiwa baada ya kukiri kosa la kuua bila kukusudia. Alisema kilitokea kutokuelewana kwa vijana hao lakini baada ya Halfan kumjeruhi Adam alionekana kujutia alichokifanya.

"Mshtakiwa alionekana kujutia alichokifanya, alitoa shati lake na kusaidia kidonda cha marehemu kisivuje damu nyingi, kwa hiyo hapo inaonesha kabisa mshtakiwa hakuwa na dhamira ovu.

"Halafu kipindi kile ni kipindi cha kukuwa kwa vijana, kwa hiyo walitaka kuoneshana ubabe na sio kipindi cha kutumia busara kutokana na umri wao kwa mantiki hiyo mshtakiwa hakuwa na dhamira ovu," alisema Shaidi Pia alisema kwa kipindi cha miaka mitano aliyokaa gerezani kuanzia Machi 12, 2015 hadi jana, kama kuna cha kujifunza basi amejifunza na kama hamna basi atakuwa anajipalia makaa katika maisha yake. "Mahakama inakuachia kwa masharti kwa kutokuenda kosa lolote kwa kipindi cha miaka miwili," alisema Shaidi.

Akisoma maelezo ya awali, Wakili wa Serikali Mwandamizi, Mwanaamina Kombakono, alidai kwamba Machi 12, 2015 mshitakiwa akiwa eneo la Manzese ndani ya Wilaya ya Kinondoni, Dar es Salaam, alikuwa akicheza kamali pamoja na Adam.

Alidai wakati wanaendelea kucheza, mshtakiwa alianza kumdai Adam fedha zake na Adam alikataa kumlipa na kisha kumsukuma, ndipo Halfan alipata hasira akamchoma na kisu shingoni.

Alidai baada ya kumjeruhi akiwa ana vuja damu nyingi, mshtakiwa na watu wengine walimpeleka Adam Hospitali ya Taifa Muhimbili na walipofika tayari alikuwa ameshapoteza maisha.

Kombakono alidai uchunguzi wa kitabibu ulifanyika katika mwili wa marehemu na ripoti ikatoka kwamba sababu ya kifo chake ni kuvuja damu nyingi. Mshtakiwa akiwa Kituo cha Polisi Magomeni kwa ajili ya kuchukua Pf3 alifanyiwa mahojiano ya onyo ambapo alikiri kutenda kosa hilo.

Hakimu Shaidi alimweleza mshtakiwa kwamba ana mtia hatiani kwa sababu amekubali kuua bila kukusudia, ambapo Kombakono aliomba adhabu stahiki itolewe kwa sababu ni maisha ya mtu yamepotea.

Baada ya Kombakono kusema hivyo, Wakili wa mshitakiwa, Harrison Mposi, aliiomba mahakama impunguzie adhabu mshtakiwa kwa sababu tayari ameshakaa gerezani miaka mitano.

Pia alidai kuwa mteja wake hakuisumbua mahakama na wamekubali kosa na pia mshtakiwa anaonekana kujutia kosa lake kutokana na kuhangaika kumpeleka marehemu hospitali na kwenda kuchukua Pf3 polisi kwa ajili ya matibabu.

# Kinana ashauri sheria fursa uchumi

**Na Mwandishi Wetu,**
KIGOMA

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Tanzania Bara, Kanali Mstaafu Abdulrahman Kinana, amesema umefika wakati kwa mamlaka mbalimbali za serikali kuweka mazingira mazuri ya Watanzania kufanya shughuli za kiuchumi katika Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ambako Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) imejumuishwa.

Amesema hakuna sababu ya kuwapo kwa vikwazo vingi ambavyo vitasababisha wananchi kushindwa kutumia fursa zilizoko kwenye jumuiya hiyo huku akisema Tanzania imebahatika kupakana na nchi nane jambo ambalo ni fursa kubwa kiuchumi.

Akizungumza jana mbele ya wana CCM na wananchi wa Kigoma, Kinana ambaye alikuwa mkoani hapa kwa ziara ya kikazi, alisema hivi karibuni DRC imejiunga na EAC hatua ambayo imepanua fursa ya soko katika eneo la jumuiya hiyo.

"Juzijuzi kulikuwa na mkutano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wakajiunga pale. Congo DRC ukubwa wake ni mara mbili ya Tanzania.

Idadi ya watu wake ni mara mbili yetu sisi. Mahitaji yao ni mara nne yetu na utajiri wao mara 20 ya sisi. Sasa kitu gani unataka zaidi ya hilo, ni fursa kubwa.

"Kuna sheria inaitwa sheria ya Afrika Mashariki ya ushuru wa forodha ambayo inarahisisha biashara kati ya nchi wanachama na ukisoma mkataba wa ushirikiano wa nchi wanachama kuna sheria nyingine inaitwa sheria ya kuruhusu watu kutoka nchi moja kwenda nyingine, mzigo kutoka nchi moja kwenda nyingine na watu wanaotaka kufanya kazi kutoka nchi moja kwenda nyingine," alisema.

"Kwa hiyo kazi ya wabunge pamoja na viongozi ni kuwaelimisha wananchi kuhusu fursa zilizomo na namna Sheria ya Jumuiya ya Afrika Mashariki inayotoa nafasi kwa watu kufanya shughuli zao na biashara ya mipkani, Tanzania ina bahati kubwa kwani inapakana na nchi nane.

"Tuna mipaka na Kenya, Uganda, Rwanda, Burundi, Malawi, Zambia, DR Congo, kila mahali tuna mipaka na watu wanafaidi biashara ya mipakani, hivyo serikali kazi yake ni kurahisisha watu kutembea si kumpiga breki kila mahali.

Watakuja Wakongomani kuja kununua vitu Kigoma, halafu unamuuliza Mkongomani umekuja kufanya nini Kigoma?

"Unadhani atarudi tena, hawezi kurudi au anafika Kigoma swali la kwanza unamuuliza ataondoka lini. Kwa wale mnaokwenda Hongkong naamini mpo hapa, ukifika Hongkong huulizwi utaondoka lini bali wanaangalia Pasipoti yako, wanapiga muhuri wa siku 90 yaani miezi mitatu kisha unaendelea na shughuli zako, tumia fedha zako, nunua unachokitaka ondoka.

"Niwaambie mimi ni Msaidizi wa Rais najua msimamo wa Rais. Rais anataka kuondokana na sheria zote zinazoleta vikwazo katika shughuli za wananchi, kazi yangu na viongozi wengine ni kumpa moyo Rais kumwambia hiyo njia unayokwenda ni sawasawa," alisema.

Kinana alisisitiza kwamba baada ya kumaliza ziara yake, atakwenda kumwambia Rais Samia Suluhu Hassan kwamba wananchi wa Mkoa wa Kigoma wamemwambia kanyaga, apeleke bungeni sheria za hovyo ili zifutwe.



Waziri wa Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula (kushoto), akizungumza na mkazi wa Pangani, mkoani Pwani, alipomaliza kuhutubia mkutano wa hadhara wa kupokea na kukabidhi taarifa ya uchunguzi wa mgogoro wa ardhi eneo la Pangani, mkoani humo juzi. **PICHA: WANMM**

# Waziri awataka wanaonunua ardhi kufanya uhakiki kwanza

**Na Munir Shemweta,**
KIBAHA

WAZIRI wa Ardhi, ,Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amewataka wananchi wanaonunua ardhi kufanya uhakiki kupitia ofisi za halmashauri sambamba na kufanya uchunguzi kwa maeneo yaliyo na hati.

Dk. Mabula alisema hayo juzi mjini hapa alipokwenda na Waziri wa Uvuvi na Mifugo, Mashimba Ndaki, kupokea na kukabidhi taarifa ya uchunguzi wa mgogoro wa ardhi katika eneo la kiwanja namba 34 Pangani, Kibaha.

Katika kiwanja hicho chenye ukubwa wa hekta 1,037 kinachomilikiwa na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, imebainika kuwa wananchi 1,002 wamevamia na kufanya shughuli za kibinadamu

Kamati, katika uchunguzi wake, iliwahoji wananchi wavamizi 1,156 katika mitaa ya Kidimu, Lumumba na Mkombozi na kuwasikiliza, kuwahoji na kupokea vielelezo mbalimbali kutoka kwa wananchi wavamizi 1,002 huku 154 kati yao wakibainika kutokuwa na nyaraka zozote za namna walivyopata maeneo kwenye eneo hilo.

Akisoma taarifa ya kamati ya uchunguzi, Katibu wa Kamati ambaye ni Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Pwani, Hussein Sadick, alisema katika mahojiano na wananchi hao, 403 walikiri kuvamia kwa kujikatia vipande vya ardhi.

Pia alisema watu 46 walidai kupewa vipande vya ardhi na wavamizi waliotangulia na wananchi sita walidai walirithi maeneo hayo. Hata hivyo, wavamizi hao wamefanya maendelezo pasipo kupata kibali cha ujenzi kutoka halmashauri kama taratibu zinavyoelekeza.

Kwa mujibu wa Sadick, historia ya eneo hilo ilianza mwaka 1982 kwa wizara kuomba eneo la kuzalisha mitamba kwa ajili ya kuhudumia Kanda ya Mashariki na hekta 4,000 kutwaliwa wakati wananchi waliokuwa wakiishi eneo hilo walilipwa fidia kwa awamu tofauti.

"Eneo lilipatikana kihalali na wizara na mwaka 2007 wananchi walivamia ambapo tathmini ya kamati ilibaini uwepo nyumba zilizojengwa kwa tope au mabati, nyumba zisizokamilika au chumba kimoja pamoja na zile zenye makazi," alisema Sadick. Akizungumza katika mkutano wa hadhara na wananchi wa mtaa wa Lumumba kata ya Pangani, Waziri Mabula alitoa rai kwa wananchi wote wanaonunua ardhi kufanya uhakiki kabla ya kununua kupitia ofisi za Halmashauri na kufanya uchunguzi kwa maeneo yaliyo na hati.

Kuhusu mgogoro katika eneo la Pangani, Waziri Mabula alisema katika eneo hilo ilibainika uwapo wa wavamizi waliounda magenge ya kutapeli wageni kutoka nje ya Kibaha hasa kutoka mkoa wa Dar es Salaam na kujifanya wamiliki wa asili katika maeneo waliyovamia.

Dk. Mabula alielekeza wananchi wote waliouziwa ardhi ndani ya Kiwanja Na. 34 Pangani kuwafungulia mashtaka ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu wale wote waliowauzia ardhi pamoja na walioshirikiana nao kufanya mauzo hayo.

Pia alitaka wavamizi wote waliotumia au kuandaa nyaraka za kughushi wachukuliwe hatua za kisheria kwa kusababisha uvamizi kwenye maeneo yenye miliki za watu wengine.

# Tanzania yapaa kimataifa uhasibu, ukaguzi

**Na Joseph Mwendapole**

TANZANIA ni miongoni mwa mataifa yanayoheshimika duniani kwenye fani ya uhasibu na ukaguzi pamoja na Nigeria zinazoongoza kwa kutumia viwango vya kimataifa vya uhasibu.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu Tanzania (NBAA), Pius Maneno, alipozungumza jijini Dar es Salaam kuhusu maadhimisho ya miaka 50 ya kuanzishwa kwa bodi hiyo yaliyoanza mwezi uliopita na yanatarajiwa kufikia kilele Novemba, mwaka huu.

Alisema miongoni mwa mafanikio makubwa ya NBAA ni kusifika kimataifa kiasi cha mataifa mbalimbali kuja nchini kujifunza masuala ya uhasibu na ukaguzi wa hesabu.

"Katika mafanikio ya kimataifa, sisi tumekuwa wanachama wa Shirikisho la Wahasibu Duniani (IFAC) na ni mwanachama mwanzilishi wa Shirikisho la Wahasibu Afrika (PAFA). Tanzania ni moja ya nchi zinazoheshimika sana duniani kwenye masuala ya uhasibu na ukaguzi," alisema.

"Afrika kuna nchi mbili tu Afrika, Tanzania na Nigeria, zinazotumia viwango vya kimataifa vya uhasibu na ukizungumza chochote hata kwenye mkutano wa IFAC, utaambiwa nenda Tanzania ukajifunze," aliongeza.

Maneno alisema kutokana na umahiri huo, Tanzania imeingia kwenye makubaliano ya miaka mitano na serikali ya Msumbiji kwa ajili ya kuwafundisha watumishi wake utawala bora katika usimamizi wa fedha.

Alisema wataalamu hao wamekuwa wakifundishwa hapa nchini na wakati mwingine wataalamu wa Tanzania wanalazimika kwenda nchini humo kwa ajili ya kutoa mafunzo hayo.

"Tunawafundisha Msumbiji kwa sababu wanataka kuwa kama sisi, Malawi, Zambia nao wamekuja wanataka tushirikiane kwenye eneo hili la uhasibu na ukaguzi ili waweze kuwa kama sisi," alisema mkurugenzi huyo.

Alisema katika shamrashamra za miaka 50 tangu kuanzishwa kwake, NBAA imeandaa shindano la uandaaji wa hesabu bora kwa kampuni, taasisi na mashirika mbalimbali.

Mkurugenzi huyo pia alisema wameandaa mashindano mbalimbali ambapo washindi watajizolea zawadi akitaja moja ya mashindano hayo kuwa ni kwa yule atakayeandaa hesabu bora.

Alisema kampuni, wizara, idara za serikali, halmashauri zinaalikwa kuleta hesabu zao zilizokaguliwa na zilizotayarishwa kuanzia mwezi uliopita hadi Novemba ambazo watazichambua na mshindi aliyetengeneza hesabu vizuri atapata zawadi.

Maneno alisema kwenye shamrashamra hizo mbali na tuzo hizo kutakuwa na mkutano mkuu wa wahasibu ambao hufanyika kila mwaka na watazungumzia masuala mbalimbali yanayohusu taaluma ya uhasibu.

"Tutajadili masuala mbalimbali yanayohusiana na maslahi ya umma na pia namna gani ya kuendeleza taaluma hii ya uhasibu na ukaguzi wa hesabu na kwenye mkutano huo tutaangalia maadili ya taaluma yetu," alisema.

Alisema katika miaka yake 50, NBAA imefanya mambo mengi makubwa ikiwamo kusajili wahasibu na wakaguzi na mpaka sasa waliofaulu mitihani ya bodi hiyo wanafikia 26,000 na kati ya hao, 12, 000 walifaulu katika ngazi ya CPA na 14,400 katika ngazi ya watunza vitabu vya hesabu.

"Pia tumesajili kampuni 450 za kutengeneza hesabu na ukaguzi haya ni maendeleo makubwa sana ndani ya miaka 50 ya NBAA, tumetunga viwango vya kutayarisha hesabu za fedha kwa sekta binafsi na kwa sekta ya umma," alisema.

Kadhalika, alisema wamefanikiwa kutengeneza kanuni za maadili ya wahasibu na wakaguzi na kuandaa semina na makongamano kila mwaka kitaifa na kimataifa.

Alisema mwaka jana pekee NBAA ilifanikiwa kuandaa mikutano zaidi ya 17 kwa wanachama wake pamoja na mashirika ikiwamo Benki Kuu Tanzania (BoT), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Alisema wamejenga kituo cha taaluma maeneo ya Bunju nje kidogo ya Jiji la Dar es Salaam (Accountancy Profession Center) (APC) na moja ya kumbi hizo inauwezo wa kuchukua hadi watu 1,000 na ndogondogo zinachukua watu 400 hadi 500.

Alisema kwa miaka yake yote NBAA imekuwa ikishauri serikali kuhusu mambo ya bajeti ikiwamo sehemu za kupunguza na kuongeza kodi, sehemu ya kuboresha wigo wa kodi.

Alisema wanachama wa bodi hiyo wamekuwa washauri wakuu wa wafanyabiashara na wenye kampuni kuhusu namna bora ya kutunza fedha katika makusanyo na matumizi ili waweze kulipa kodi wanazostahili.

## Watakiwa kuwafanya marafiki wafanyakazi

**Na Sabato Kasika**

WATU wenye wafanyakazi wa ndani, wametakiwa kutowabagaua, badala yake wawaheshimu na kuwafanya kama marafiki na kuwatimizia mahitaji yao, ili kuepuka matukio mabaya ambayo yamekuwa yakitokea katika nyumba zao, yakitajwa kusababishwa na wafanyakazi hao.

Mkurugenzi wa taasisi isiyo ya kiserikali inayohudumia watoto wa kichwa kikubwa, mgongo wazi na wenye mahitaji maalum ya Kaya Foundation ya jijini Dar es Salaam, Annapili Ngome, alitoa wito huo juzi.

Annapili, alikuwa miongoni mwa washiriki wa semina ya kuongeza ushiriki wa wanawake katika nafasi za maamuzi, ilioandaliwa na Kituo cha Sauti ya Jamii Kipinguni, na kusema wafanyakazi hao wana haki sawa na watu wengine.

"Mtu ambaye ana mfanyakazi wa ndani, anatakiwa kuheshimiwa, kumfanya kuwa rafiki, ili kuepusha migogoro, kwani kuna matukio mengi mabaya yanatokea huku wafanyakazi hao wakidaiwa kuwa chanzo," alisema Ngome.

Mkurugenzi huyo alitaja baadhi ya haki za mfanyakazi wa ndani kuwa ni kulipwa mshahara, mkataba wa kazi, likizo, kupendwa, kusaidiwa majukumu, kulindwa, kuheshimiwa, kusikilizwa na kuchukuliwa kama mwanafamilia.

"Bahati mbaya, kwenye baadhi ya familia hayo yamekuwa hayafanyiki, hali ambayo ni hatari, hivyo wito wangu ni kwamba tuwatimizie mahitaji yao na kutowabagua, kwani nao wana haki," alisema.

Alisema, katika baadhi ya familia, mfanyakazi wa ndani anatengwa mbali wakati wa chakula na pia analazwa sehemu mbaya, kudharauliwa na watoto wa bosi wake, hali ambayo amebainisha inaongeza chuki. "Si vibaya bosi unapowanunulia watoto wako nguo, mnunulie pia, ukitoka na familia yako, ambatana naye, unapokula na watoto wako mezani naye awepo, pia mfundishe mambo mengi kuhusu maisha," alisema. Mweka hazina wa taasisi inayojishughulisha na uwezeshaji wa wanawake kijamii na kiuchumi ya Nyota TZ, Mwanakombo Ramadhan, alisema wafanyakazi wa ndani ni watu muhimu na faida katika familia.

Iwapo mfanyakazi wa ndani hatabaguliwa, atakuwa wazi kukushirikisha mambo ambayo hata wazazi au marafiki zake hajawahi kuwaambia, atafanya kazi zote kwa moyo wa kupenda na uhiyari," alisema Mwanakombo. Aliongeza kuwa atakuwa anajituma kufanya mambo ambayo si kazi zake ila tu ni kwa sababu anajua anamsaidia rafiki yake, na kwamba kuna ujuzi ambao unao utaanza kuambukizwa ndani yake.

"Lakini maono, tabia, na shauku ulivyonavyo vitaanza kuambukizwa ndani yake na atajiona anawajibu wa moja kwa moja wa kukuunga mkono, pia atawatumikia watoto wako, hata kama haupo watoto hawataona kupungukiwa, kwani ataishi nao kwa upendo wa hali ya juu," alisema. Alisema, kwa njia hiyo, mfanyakazi atamjali mtoto na kujua nini bosi wake anapenda na atamtendea mema, na kwamba ataona ana wajibu wa moja kwa moja wa kulinda na kutunza mali za bosi wake.

Mkurugenzi wa Kituo cha Sauti ya Jamii, Seleman Bishagazi, alisema, wamefanya semina hiyo kwa lengo la kutaka kuhakikisha wanawake na wasichana wanaondokana na unyanyasaji na ukatili wa kijinsia.

"Kituo chetu kimepata ufadhali kutoka Women Fund, ili kuendesha semina kwa ajili kuwajengea uwezo wanawake na wasichana waweze kuondokana na vikwazo vya kiuchumi, kijamii na hata kisiasa," alisema Bishagazi.



Mkuu wa Wilaya ya Korogwe, Basila Mwanukuzi, akichimba msingi wa Shule ya Sekondari Mgwashi, ambao ujenzi wake umecheleweshwa kwa muda wa miezi 10, huku akishuhudiwa na Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba (kushoto), alipofanya ziara wilayani humo, juzi. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

## Jela maisha kunajisi mtoto miaka 5

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MKAZI wa Kijiji cha Mandi, Babati mkoani Manyara, Paschal Daniel (23), amehukumiwa kifungo cha maisha gerezani baada ya kutiwa hatiani kwa kosa la kumbaka mtoto wa miaka mitano (jina limehifadhiwa).

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Babati, Victor Kimario. Mshtakiwa alidaiwa kutenda kosa hilo Julai 3, mwaka huu katika Kijiji cha Mandi.

Kimario, alisema mahakama imemtia hatiani mshtakiwa baada ya kusikiliza pande zote mbili, yaani upande wa mashtaka na upande wa utetezi ambapo upande wa utetezi mshtakiwa hakuwa na mashahidi alijitetea mwenyewe na upande wa mashtaka ulikuwa na mashahidi sita.

Hakimu Kimario, alisema katika shauri hilo namba 110 la mwaka 2022, kosa alilotenda lilikiuka kifungu cha 130 (1) (2) (e) na kifungu cha 131 (3) cha Sheria ya Kanuni za Adhabu Sura ya 16 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2019.

Alisema, kati ya mashahidi sita, mmoja alikuwa mtoto aliyeathirika na tukio na shahidi mwingine alikuwa kaka yake ambaye alieleza mahakama kuwa walikutana na mshtakiwa wakiwa wanaenda dukani kununua mahitaji ya msingi.

"Shahidi huyo alidai aliwalaghai na kuwapa Sh. 1,000 ili wanunue pipi na alimpeleka mtoto huyo shambani. Kaka yake alipoona harudi alipiga kelele ili asaidiwe kumpata mdogo wake," alisema Kimario

Aidha, alisema suala la kuonekana mshtakiwa akiwa na mtoto huyo hakubisha na jambo la kuwapa Sh. 1000 hakukataa ila alidai kuwa aliondoka na Sh. 500 na kwamba baadaye alikamatwa na kupelekwa ofisi ya kijiji cha Mandi.

Vile vile, alisema shahidi mwingine aliyetoa ushahidi ambao nao umemtia hatiani ni taarifa ya Daktari aliyemfanyia vipimo ambapo vilithibitisha kuwa alimbaka.

Awali, Wakili wa Serikali, Grace Mgaya, alidai kuwa mshtakiwa hana kumbukumbu za makosa ya nyuma lakini aliiomba mahakama hiyo itoe adhabu kali ili iwe fundisho kwa watu wengine.

Mshtakiwa alipopewa nafasi ya kujitetea, alidai kuwa aliwahi kupata ajali na kuumia ubongo wa kati, hivyo siku zote kichwa kinamuuma na kwamba hatakiwi kukaa kwenye kelele na kuomba mahakama imwachie huru.

Aliongeza kuwa ana matatizo ya moyo na sukari yanamsumbua na ana wadogo zake wanamtegemea hivyo aachiwe huru.





# Bunge lataka kasi katika ujenzi viwanja vya ndege

**Na Magdalena Jackson,**
SJMC

KAMATI ya Bunge ya Uwekezaji na Mitaji ya Umma (PIC) imeagiza kuharakishwa kwa mchakato wa ujenzi wa viwanja vya ndege nchini ili kuongeza tija kwenye Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Tanzania (TAA).

Mwenyekiti wa PIC, Jerry Silaa, alisema hayo jana baada ya kamati hiyo kupokea taarifa kutoka mamlaka hiyo na kueleza kuwa kamati imeridhishwa na utendaji wa TAA ambayo kwa sasa inasimamia viwanja 58, nchini.

Silaa alisema mambo ya kufanywa ni kuharakisha mchakato wa kurejesha mamlaka ya ujenzi na usimamizi wa viwanja vya ndege.

Pia alisema mamlaka husika zinapaswa kuhakikisha viwanja vyote vinapimwa na kupata hati ili kupunguza uvamizi na kutengeneza mpango mkakati endelevu.

"Mamlaka ya viwanja vya ndege inapaswa kuandaa mpango mkakati wa kuboresha viwanja kwa kuzingatia viashiria vingine vya kiuchumi, kama vile abiria, mizigo, utalii, bandari, biashara na kodi," alisema.

Alisema kuwa majukumu hayo yakitekelezwa na kuzingatiwa itaisaidia mamlaka kuwa na uwezo mkubwa wa kuleta tija kwenye shirika pamoja na taifa kwa ujumla.




Mkazi wa Kijiji cha Mbande, Wilaya ya Kongwa, akitumia tela linalokokotwa na ng'ombe kama nyenzo ya usafiri wakati akitafuta wateja wa maji, kijijini hapo jana. Dumu moja lenye maji aliliuza kwa bei ya Sh. 400/- hadi Sh. 500/-. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Wanawake waonywa kuhusu mikopo

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

MWENYEKITI wa Jukwaa la Wanawake wa Mkoa wa Dodoma, Mary Mabhaye, amewataka wanawake wanaochukua mikopo kutoka taasisi za kifedha kutokuwa watumwa kwa kushindwa kurejesha kwa wakati. Mabhaye alitoa ushauri huo jana jijini alipokuwa akizungumza na wanawake kwenye semina ya jukwaa hilo iliyolenga kuwainua kiuchumi.

Alisema wanawake wengi wamekuwa wakianzisha vikundi kwa malengo ya kukopa fedha ili waondokane na utegemezi na umasikini lakini matokeo yake wakati wa kurejesha wanageuka kuwa watumwa.

Wanawake hao wasiorejesha mikopo, alisema wamekuwa watumwa na kusababisha hata familia zao kushindwa kulea kutokana na kutumia muda mwingi wa kuishi kwa kujificha.

"Tatizo walilonalo baadhi ya wanawake wanaochukua mikopo hawana elimu ya kutosha juu ya ujasiriamali, badala yake wanajikuta wakiangukia kwenye matumizi yasiyokuwa na tija ambapo hujikuta wakishindwa kurudisha mikopo hiyo kwa wakati," alisema.

Pamoja na hayo, aliwashauri wanawake hao kujitokeza kugombea kwenye nafasi za uongozi mbalimbali hapa nchini ili kujikwamua kiuchumi.

Alisema wakijitokeza watapata fursa mbalimbali nchini ambazo zitakazowainua kiuchumi na kuwasaidia wanawake wengine katika suala zima la kujipatia maendeleo.

Ofisa Biashara wa Jiji la Dodoma, Donatila Donisi, alisema wanawake wamekuwa na mchango mkubwa katika kuleta maendeleo kwa lengo la kukuza uchumi nchini hivyo wamejiandaa vyema kutoa elimu kwenye vikundi vyao. "Halmashauri ya Jiji watatoa elimu hususani katika biashara wanazofanya kwa lengo la kurasimisha ili kuwasaidia katika kutambulika na kupata masoko ya kufanyia biashara kwa urahisi.

"Sisi kama jiji hususani kwenye ofisi ya biashara tutakuwa tayari kwa ajili ya kuwapa elimu mbalimbali ikiwemo umuhimu wa kurejesha mikopo kwa wakati pamoja na ulipaji wa kodi ili kuwezesha serikali kufanya maendeleo," alisema.

Nao washiriki wa mafunzo hayo, Juliana Sakaine na Ailen Salvatory, walishauri wajasiriamali kutengeneza bidhaa zitakazowafanya kuingia kwenye soko la ushindani ndani na nje ya nchi.

Walisema kuwa tatizo lililopo kwenye bidhaa nyingi zinazotengenezwa hazina viwango na zilizo nyingi zinakosa masoko kutokana na watu kuendelea kununua zinazotoka nje ya nchi.

# Watakiwa kutumia kadi kufanya ununuzi bidhaa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WATANZANIA wametakiwa kujenga tabia ya kufanya ununuzi kwa kutumia kadi ya benki ya 'Tembocard' ili kujiepusha na kutembea na maburungutu ya fedha yanayovutia wahalifu.

Meneja wa Benki ya CRDB Kanda ya Kati, Chabu Mshwaro, alisema hayo jana kwenye uzinduzi wa promosheni ya matumizi ya 'Tembocard' iliyopewa jina la 'Tisha na Tembocard', uliofanyika jijini hapa.

Alisema mtu akitembea na maburungutu ya fedha anawavutia wahalifu na kuhatarisha maisha yake.

Meneja huyo alisema bado Watanzania wengi hawana mwamko wa kutosha juu ya matumizi ya kadi.

"Kitu hiki kimesababisha kutokutumia vizuri huduma zote ambazo zinapatikana kwa njia ya kadi, hususani malipo,"alisema.

Alisema kutokana na hali hiyo wamezindua promosheni hiyo itakayoendeshwa kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia ilivyozinduliwa rasmi kitaifa Dar es Salaam Agosti 18, mwaka huu.

"Promosheni hii ina lengo la kuwahamasisha wateja na watanzania kujenga utamaduni wa kutumia kadi zao kufanya manunuzi na malipo ya huduma huku wakijishindia zawadi," alisema.

Alitaja zawadi hizo ni fedha taslimu kila mwezi kwa wateja watatu ambapo watajishindia Sh.milioni moja kwa mshindi wa kwanza, wengine washindi wawili watapata Sh. 500,000.

"Na kubwa zaidi ni safari ya kwenda nchini Qatar iliyolipiwa kila kitu kwa wateja wanne wa TemboCard, washindi ni wale tu watakaokuwa na miamala mingi kupitia kadi zao za TemboCard,"alisema.

Alisema kadi hizo zinatumika kupitia ATM, matawi, CRDB Wakala, mashine za malipo (POS) na kufanya ununuzi na malipo kwa njia ya mtandao ndani na nje ya nchi.

Meneja Biashara CRDB Kanda ya Kati, Jane Maganga, alisema promosheni hiyo ni ubunifu wa CRDB katika kuwarahisishia wateja wake kupata huduma mbalimbali.

"Hii promosheni ya 'Tisha na Tembocard' ni shindano ambalo litampa mabadiliko mteja, atakuwa akihitaji huduma au bidhaa anatumia kadi yake kuchanja tu na kulipia badala ya kutoa burungutu la fedha,"alisema.





# 'Hakuna anayedai malipo sensa Zanzibar'

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KAMISAA wa Sensa Zanzibar, Balozi Muhammed Hamza, amesema malipo kwa makarani na wasimamizi wa sensa yameshafanyika yote na hakuna deni wanalodai.

Balozi hamza, amesema changamoto iliyojitokeza katika mchakato huo ni kwa baadhi ya makarani kutopata fedha zao kwa sababu ya kukosea namba za akaunti zao.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Mazizini mjini Unguja.

Kamisaa, huyo alisema changamoto iliyojitokeza kwa baadhi ya makarani na wasimamizi wa fedha hawajapokea na baada ya kufuatilia imegundulika kuwa walikosea namba za akaunti zao.

Pia, alisema sensa ya watu na makaazi imefanyika vizuri na hivi sasa wanaendelea na sensa ya majengo, hivyo akawataka wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa makarani wa sensa ya majengo ili kuwa na idadi ya majengo kwa maendeleo.

Alisema, sekta ya ujenzi ina mchango mkubwa katika maendeleo, hivyo wananchi wasiwe na hofu ya kutoa taarifa katika sensa hiyo.

Sensa ya mwaka huu, imeongeza ufanisi na kupunguza gharama kwa sababu anuani za sensa na makazi na sensa ya majengo vimeenda sambamba.

Naye Mkurugenzi wa Viwango, Uratibu wa Takwimu na Utafiti kutoka Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Bakari Kitwana Makame, alisema hadi sensa ya watu na makazi inakamilika, vishikwambi walivyokabidhiwa makarani na wasimamizi viko salama.

"Tunashukuru kuwa zoezi limekamilika hakuna matukio mabaya yaliotokea na vishikwambi vyote vipo salama," alisema.



Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdullah (kushoto), akiwa na Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda, Omar Said Shaaban, wakiangalia karafuu, walipofanya ziara ya kukagua vituo vya kuuzia zao hilo, Kisiwani Pemba jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hemed ataka kasi ujenzi matangi maji

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais, Hemed Suleiman Abdulla, amewataka makandarasi wanaojenga matangi ya maji kuongeza kasi ili kukamilisha kwa muda waliokubaliana katika mikataba.

Hemed, alisema hayo jana katika ziara ya kukagua miradi ya ujenzi wa matangi matano ya maji yenye uwezo wa ujazo tofauti inayojengwa kwa pesa za ahueni ya UVIKO- 19 kisiwani Pemba. Alisema, serikali ya haitaongeza muda wa ujenzi wa miradi hiyo kinyume cha makubaliano ambayo yamefikiwa kwenye mkataba husika.

"Serikali haitavumilia ucheleweshaji wowote ambao utafanywa na mkandarasi anayejenga mradi wa serikali kwa maslahi ya taifa na wananchi kwa ujumla," alisema.

Kwa mujibu wa Hemed, serikali imejipanga kutatua changamoto ya upatiakanaji wa maji safi na salama kwa Unguja na Pemba, hivyo ni vyema makandarasi wakaongeza kasi katika ujenzi ili kuhakikisha serikali inafikia malengo iliyojiwekea kwa wananchi wake.

Hemed, alisema serikali haitapokea tangi lolote lilil chini ya kiwango, hivyo alimtaka mshauri elekezi kusimamia vyema ili kuhakikisha matangi hayo yanajengwa kwa kiwango na yanamalizika kwa wakati uliopangwa. Aidha, aliutaka uongozi wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini kupitia Mamlaka ya Maji Zanzibar (ZAWA), kuchimba visima na kusambaza mabomba mapema ili yatakapokamilika matangi hayo, yaanze kutumika mara moja.

"ni vyema kuchimba visima mapema pamoja na kusambaza mabomba ya maji ili matangi yakimalizika tu yaweze kutumika na sio tukasubiri mpaka matangi yakamalizika ndio tukaanza kuchimba visima na kusambaza mabomba hii sio sawa wananchi wanashida sana ya maji"alisema

Naye Mkurugenzi mkuu wa mamlaka ya maji Zanzibar (ZAWA), Dk Salha Mohamed Kassim, alisema miradi inayojengwa ni utekelezaji wa ahadi ya mheshimiwa rais kwa wananchi wake ya kuwaondolea changamoto zote hasa suala la upatikanaji wa maji safi na salama kwa Unguja na Pemba

Pia, alisema wizara kupitia ZAWA, itahakikisha inasimamia miradi yote inayojengwa na serikali ikiwamo ya fedha za ahueni ya UVIKO - 19 inajengwa kwa viwango na kumalizika kwa wakati kwa maslahi ya wananchi.

# SMZ yawapongeza wadau maendeleo

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MAKAMU wa Kwanza wa Rais Zanzibar, Othman Masoud Othman, ameshukuru juhudi zinazochukuliwa na washirika wa maendeleo katika kukuza demokrasia na utawala bora nchini.

Othman, alitoa shukrani hizo jana wakati wa mazungumzo yake na ujumbe kutoka Taasisi ya Demokrasia (NDI), Shirika la Kimataifa la Maendeleo la Marekani (USAID), na Jumuiya ya Wanawake Wenye Ulemavu Zanzibar (JUWAUZA), uliofika ofisini kwake Migombani, kwa lengo la kubadilishana mawazo.

Alisema, serikali za Zanzibar pamoja na ya Muungano zinahitaji kushikamana na wahisani pamoja na washirika wa maendeleo katika kufanikisha fursa muhimu zikiwamo za kujenga demokrasia na utawala bora, ambazo kwa sasa taifa limekuwa likizihitaji.

Othman, alizitaja taasisi hizo pamoja na serikali ya Marekani kwamba hazikuacha kushikamana na Zanzibar pamoja na Tanzania kwa ujumla katika kufanikisha vipaumbele mbalimbali na kwamba kwa sasa fursa bado ipo ya kusaidiana katika kujenga demokrasia na utawala bora, ili kutekeleza haja ya maendeleo ya kweli nchini.

Akipokea ripoti kuhusu utafiti juu ya utekelezaji wa maridhiano ya kisiasa na Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) Zanzibar kutoka JUWAUZA, Othman alisema taarifa za utafiti huo zimekuja wakati mwafaka na juu ya haja ya kuunda kikosi kazi kuraratib na kusimamia utekelezaji huo.

"Tunachoweza kubaini sasa ni dhamira ya utekelezaji wa mapendekezo ambayo yanatoa mwangaza wa kujenga mariadhiano ya umoja wa kitaifa katika ngazi zote na hilo linahitajika sana kwa sasa," alisema Othman.

Akiwasilisha taarifa za utafiti huo, Mtafiti kutoka JUWAUZA, Rashid Aziz, alisema kuna umuhimu wa kuwa na mjadala wa pamoja wa kutathmini mwenendo wa SUK, kwa kuzingatia fursa, changamoto na mustakabali wake, sambamba na hatua ya vyama vinavyoshiriki, kufanya mashauriano ya ndani ili kubaini utayari na uwezekano wa kuongeza wigo katika kuijengea ufanisi na mafanikio zaidi.

Alitaja maeneo yaliyoguswa katika utafiti huo kuwa ni pamoja na muundo wa SUK; utoaji wa nafasi za ajira kwa umma, mabadiliko ya taratibu za uchaguzi, upatikanaji wa vitambulisho na vyeti vya kuzaliwa, uchumi wa buluu na kusahauliwa kwa baadhi ya makundi ya kijamii.



**HEMANT**
UKURASA 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII

BT
BURUDANI TELE



# KUMBE KWELI Wabongo tofauti na majuu



KUMBE kweli! Ndivyo mashabiki wa muziki walivyojikuta wakisema pale walipopokea taarifa ya kupata mtoto wao wa kwanza kwa wanamuziki nyota wa Bongo Fleva, Nandy na Billnass.

Taarifa ya kupata mtoto zilianza kuzagaa mwishoni mwa wiki iliyopita, lakini Nandy kupitia Instagram yake alikanusha huku akiwacharukia wale waliokuwa wakimpongeza.

Baada ya kupita siku chache, Billnass kupitia ukurasa wake wa Instagram, aliandika ujumbe wa kumshukuru Mungu kwa kumpata mtoto wao wa kwanza wa kike.

Imekuwa desturi ya mastaa mbalimbali kuficha habari ya pale wanapopata watoto kwa nia ya kibiashara, lakini wengi wanajikuta wakishindwa kutunza siri kutokana na taarifa hizo kufichuka na kusambaa kwa kasi.

Nandy, alipojifungua tu, taarifa zilianza kusambaa mitandaoni huku baadhi ya mastaa wakimpongeza kupata mtoto. Licha ya mwenyewe kukana taarifa hiyo, lakini watu tayari walishajua kuna ishara ya aina hiyo, hivyo, hata Billnass alipotangaza rasmi halikuwa jambo jipya kwao.

Tofauti na mastaa wa Ulaya na Marekani ambao watoto wanapozaliwa wana kawaida wa kuwatangazia mashabiki zao, lakini wanapiga pesa katika kuonyesha sura za watoto zao. Katika ujumbe wake Billnass alimshukuru Mungu kwa kuwapatia zawadi hiyo ya kipekee na kuahidi kutoa sadaka kutokana na jambo hilo la furaha.

"Nakushukuru mke wangu kipenzi Nandy, kwa kuniletea mrembo na rafiki, haikuwa kazi rahisi umenionyesha wewe ni shujaa kiasi gani kuanzia mtoto akiwa tumboni mpaka muda unajifungua umepigana sana. Nimejionea namna gani mtu anaweza kuhatarisha kwa kupoteza uhai wake wakati wa kujifungua hii imefanya nizidi kukupenda, kukuheshimu na kukupa nafasi ya pekee katika maisha yangu," ameandika Billnass.

BASI SAWA

## Sholo Mwamba kuwa sawa na AY



MWANAMUZIKI mkongwe wa Singeli, Sholo Mwamba, ameshirikishwa katika ngoma mpya ya mkongwe AY na kueleza ndoto yake ya kufika mbali imeanza kutimia.

Amesema, kwa kufanya kazi na mwanamuziki huyo anayejulikana kimataifa, ni njia pekee ya kwake kufahamika na hivyo kuutangaza singeli nje ya nchi.

"Singeli Twista ni kazi iliyoandaliwa kwa hatua zote, na tunaona kabisa njia nyeupe ya kwenda kimatafa," amesema.

## D Ukingo ana jambo lake



Ni muziki wenye ladha tofauti katika Bongo Fleva, lakini unaleta raha pale unapisikiliza kwa utulivu.

Mwanamuziki Afro Hip Hop, D Ukingo ameachia video ya ngoma yake mpya iitwayo 'Something' akiwa amemshirikisha msanii wa Kizungu Talya.

"NI muziki wenye uasili wa Kiafrika na ndio maana nimekuwa tofauti na wengine, nashukuru mashabiki wamenipokea vizuri na nina deni kwao kuwaletea kazi zilizo bora," amesema D Ukingo.



## HEMANT PUNJABI AIWINDA AFRIKA MASHARIKI

MSANII mwenye asili ya India anayeishi Cotonou nchini Benin, Hemant Punjabi, ametangaza kuwa lengo lake sasa ni kuingia kwenye soko la Afrika Mashariki.

Punjabi, anayemiliki mgahawa maarufu wa Kihindi, ameliambia BT kuwa, ndiye mwanamuziki wa kwanza wa India kuachia wimbo wa Kiafrika-India unaoitwa Mon BB, akimshirikisha Vano Baby, mwana muziki wa Benin.

Wimbo huo umetazamwa mara 395,000 kwa kipindi cha miezi mitano.

"Wimbo wangu uliofuata ni Wa Dû Vé ulitolewa mwezi uliofuata pia nikaachia Cheri Main Ter ambao natumia mtindo wa Indo-Afro-Pop uliochanganya maneno ya lugha mbili. Natamani niendelee kupenya hapa Afrika na zaidi huko Afrika Mashariki," amesema Hemant Punjabi.



## Dick Flavour kutambulisha video

"Nitakitumia' kwa mbwembwe

MSANII wa muziki wa kizazi kipya, Dick Flavour, atatambulisha video ya wimbo wake mpya 'Nitakutimia' kwa mbwembwe za aina yake.

Dick Flavour amesema video hiyo ambayo imetengenezwa katika ubora zaidi kuliko nyimbo zingine za singeli, itawekwa hadharani wiki ijayo baada ya kufanya ziara katika vituo vya habari.

"Utambulisho wa video ya wimbo wangu mpya utakuwa wa kipekee, nimejipanga kuhakikisha kila mtu anakuwa wa kwanza kuona kupitia vyombo vya habari na hii naifanya kuleta furaha kwa kila mtu," amesema Dick Flavour.

## Lazima Anitambue: Risasi ya shabiki wa 20 Percent

**Na Adam Fungamwango**

NI filamu ya kusikitisha, ikimhusu shabiki wa muziki wa msanii Abbas Hamisi maarufu kama 20 Percent, aliyekuwa akipigana na wenzake ambao ni mashabiki wa wasanii wengine kwa ajili ya kumtetea.

Hatimye anakuja kumpiga risasi na kufungwa.

Imechezwa na 20 Percent mwenyewe, Charles Magari, Rehema Tajiri, Cleopatra, Brigita, Kijoli, Mohju, Juma Madenge na wengineo.

Inaanza kwa kuonyesha kuwa mzee Magari anaumwa. Anamwita kijana wake wa kiume ambaye ni Madenge na kumweleza kuwa huenda asipone, hivyo pamoja na nyumba anayoiacha, lakini mali nyingine aliyonayo ni bastola ambayo ipo uvunguni mwa kitanda.

Madenge anajishughulisha na genge kwa kuuza nyanya, vitunguu, mbogamboga na vitu vingine vinavyofanana na hivyo.

Si tu kwamba ni shabiki wa 20 Percent pia huwa anabishana kama Yule mushabiki wa Simba na Yanga.

Na si mara moja wala mbili hupigana na mashabiki wa wasanii wengine, kila mmoja akivutia upande wake kuwa msanii wake ni bora zaidi kuliko wengine.

Madenge, hutembea na redio yake ambayo huweka kanda za msanii anayempenda. Wakati mwingine husababisha hata asifanye shughuli zingine za maana kiasi hali yake ya maisha ikabaki kuwa vile vile.

Mpenzi wake Cleo, mara kwa mara akawa anashawishiwa na wanawake wenzake amuache Madenge, badala yake atafute wanaume wengine wenye pesa.

Cleo hakukubaliana nao, akisema anamvumilia mpenzi wake kwa shida na raha. Shoga zake walimletea hadi wanaume hao laivu, lakini yeye alibaki na Madenge.

Kuna wakati wanakorofishana na mpenzi wake kutokana na tabia yake ya kuchukua pesa za kula na kununua betri kwa sababu ya kusikiliza nyimbo za 20 Percent.

Siku moja, msanii hiyo alifika Tanga mjini kwa ajili ya kutumbiza. Cleo alipojua hilo alijitahidi kumzuia kwa kila hali ili asiende kwenye onyesho. Hakufanikiwa. Madenge alitoroka na kwenda Tanga mjini.

Alipofika akakuta wasaa wa kupiga picha na msanii huyo umeisha. Yeye alichelewa. Kwa sababu anampenda akataka kulazimisha. Baunsa akamsukuma. Akatoa bastola ili ampiga baunsa. Kwa sababu hakuwa na shabaha ikampiga 20 Percent kwenye mkono wa kushoto, akakamatwa na kufunguliwa kesi ya kujaribu kuua.

Siku ya hukumu, pamoja na kujitetea kuwa yeye ni mpenzi wa 20 Percent na hakuwa na nia mbaya, lakini haikusaidiwa. Akahukumiwa miaka mitatu jela.

## NGOMA ZA 'LONGI' BADO ZINACHENGUA

**Na Adam Fungamwango**

NI ukweli usiopingika kuwa nyimbo nyingi za zamani zimekuwa na mvuto usiochuja, au kupitwa na wakati. Wanamuziki wa zamani walizungumzia mapenzi, afya, elimu, mahusiano ya kijamii, majanga, misiba, siasa na mengi matamu yakuvutia yanayowafundisha wasikilizaji .

Ndiyo maana hadi leo zinapotokea shughuli za kisiasa kama Muungano, Uhuru na nyingine, nyimbo zinazotamba ni za muziki wa zamani na dansi.

Hata unapotokea msiba wa kitaifa, nyimbo zinazochukua nafasi za maombolezo zinakuwa ni za zamani kwa sababu wao waliangazia sehemu nyingi.

Kuna baadhi ya nyimbo za zamani ambazo hakuna hata kijana mmoja wa kisasa hapa Bongo ambazo anazifahamu.

Hizi ni baadhi ya nyimbo tano ambazo zilipigwa zamani, lakini zinapendwa hata na vijana wa kizazi cha sasa.

**Rangi ya Chungwa-Nyanyembe Jazz**

Ni wimbo uliorekodiwa mwaka 1975, na bendi ndogo tu ya Nyanyembe Jazz ya mjini Tabora.

Hata hao watu wazima si wengi wanaoifahamu bendi hiyo, lakini wimbo huo umeendelea kuwa maarufu zaidi kwa miaka 47 sasa.

Ni wimbo ambao ukipigwa kwenye redio, hata watoto wanaonekana kuupenda na kuukubali.

Kwenye bendi mbalimbali nchini, kama wimbo huu haikupigwa basi hilo dansi halijaisha bado.

Ndiyo wimbo unaoombwa zaidi na mashabiki dansini, kwenye bendi zinazopiga muziki wa laivu nchini Tanzania.

**Georgina-Safari Trippers**

Huu nao ni mmoja wa wimbo maarufu sana mithili ya wimbo wa taifa. Hakuna kijana wa sasa ambaye haujui wimbo huu. Hautofautiani sana na 'Rangi ya Chungwa'. Nao unapigwa sasa kwenye bendi mbalimbali zinazopiga muziki wa laivu. 'Georgina' unashindana na wimbo huo kuombwa na mashabiki na wengi ni vijana wa kizazi cha sasa, licha ya kwamba nao ulirekodiwa mwaka 1976 na bendi ya Safari Trippers, ukitungwa na Jumanne Uvuruge na kuimbwa na hayati Marijani Rajab.

**Karubandika-Maquiz Original**

Si tu kwamba wimbo huu ni maarufu zaidi Tanzania, lakini hata nchini Kenya. Mtunzi mwenyewe Kasaloo Kyanga, kabla umauti haujamkumba, alisema kuwa alikwenda nchini Kenya na kuukuta wimbo huo unapigwa kwenye kila bendi ya laivu. Lakini alipowaambia kuwa yeye ndiye mtunzi wa wimbo huo, walionyesha shaka, lakini alipokuwa akipanda jukwaani na kuuimba, ndipo wanapokubali kwa sababu ya sauti yake ndiyo ile halisia wanayoisikia kwenye redio.

Hapa Bongo, vijana wengi wa kizazi cha sasa wanaufahamu sana wimbo huu na kuuimba mitaani, japo ulitungwa mwanzoni mwa miaka ya '90.

**Sina Makosa-Les Wanyika.**

Wimbo wa 'Sina Makosa' nao ni moja ya ngoma ambazo vijana wa kisasa hawapati hata tabu kuufahamu.

Ni wimbo maarufu sana mitaani hata kwa watoto wadogo. Kwenye bendi za laivu huu ni kipenzi zaidi kwa wasichana miaka 18 hadi 25 ambazo wamekuwa wakiuomba, kuucheza na kuuimba, unaweza ukadhani kwamba umetungwa kipindi hiki hiki cha kina Diamond, Ali Kiba na Harmonize, wakati ulitungwa mwishoni mwa miaka ya '70.

**Mtaa wa Saba-Mbaraka Mwinshehe**

Wimbo huu uliotungwa miaka ya '70, ulipata umaarufu sana kwenye miaka ya 2000, baada ya kituo cha tevevisheni cha East Afrika kuupiga, huku wachekeshaji wakiucheza.



Hii ilisababisha vijana na watoto wengi kuujua na kuanza kuuimba mitaani na hata kuigiza jinsi ya uchezaji wa wale jamaa, hivyo kuufanya uwe unapigwa hadi kwenye sherehe mbalimbali za kijamii.

Nao ni moja ya nyimbo maarufu sana za zamani zinazotambuliwa na vijana wa kizazi cha sasa.



# Portable alianzisha, anywea mwenyewe

MWANAMUZIKI aliyetokea mtaani nchini Nigeria, Portable, hatimaye ameomba msamaha kwa msanii mwenzake Davido, kutokana na maneno ya kashfa aliyoyatoa wakati wa maandalizi ya uchaguzi wa ugavana katika Jimbo la Osun.

Itakumbukwa kwamba, wakati wa uchaguzi uliopita wa ugavana katika jimbo hilo, Davido alipiga kampeni kwa mjomba wake, Ademola Adeleke kutoka PDP, huku Portable akimpigia kampeni Gboyega Oyetola, wa chama tawala cha All Progressives Congress (APC).

Katika moja ya kampeni, Portable alimpiga vijembe Davido kiasi cha kuleta tafaruku.

"Hakuna kitu kati yangu na Davido, niliitwa kwa kazi pale nikakusanya pesa, mimi na Davido hatuna ugomvi, wakati huo huo lolote litakalotokea hakuna tatizo, mimi ni mtoto wa Mungu, sipigani na mtu yeyote. Natafuta pesa. Mashabiki wa Davido watanisamehe. Samahani," alisema.



## DiCaprio, Morrone waachana

MWIGIZAJI wa Marekani, Leonardo DiCaprio na mpenzi wake Camila Morrone wameachana baada ya kuwa wachumba kwa muda wa miaka minne.

Kulingana na PageSix, DiCaprio na Morrone wametofautiana kwa muda, lakini haijawekwa wazi sababu ya mgogoro wao.

Mnamo Mei, DiCaprio alionekana akimfariji Morrone, baada ya kufanya mazungumzo yenye hisia kwenye ufukwe wa Malibu.

Haijulikani ni lini wawili hao waliachana rasmi, lakini DiCaprio ameonekana akiwa likizo peke yake huko Ulaya.

## Buju toka lini siri ikawa ya wawili?

NYOTA wa muziki kutoka Nigeria, Buju BNXN amevunja ukimya kwa kuomba msamaha baada ya video yake ya ngono kuvujishwa na anayedaiwa kuwa mpenzi wake.

Mwanamuziki huyo kupitia ukurasa wake wa Snapchat, amesema amehuzunika kwa mara ya kwanza katika maisha yake.

"Sina uwezo wa kumpenda mtu yeyote katika dunia hii huu kando na Peggy. Kabla hujanijia na chochote unachofikiria kupata chini ya jua hili," ameandika.





## Meghan akasirisikia ubaguzi

MSANII wa filamu na mke wa mwanamfalme wa Uingereza, Meghan Markle, amevishutumu vyombo vya habari vya Uingereza kwa kuwaita watoto wake jina la N' linaloshiria ubaguzi.

Malkia huyo wa Sussex, alifahamisha kero hiyo wakati wa mahojiano ya kipekee na The Cut.

"Kuna muundo halisi. Kwa nini niwapende watu hasa wanaowaita watoto wangu neno-N, niambie jinsi gani hiyo ina maana kisha nitacheza mchezo wao."

Amebainisha Markle.

Itakumbukwa kwamba mnamo Januari 2020, Prince Harry na mkewe, Markle walishtua dunia walipotangaza kwamba wanajiondoa katika utumishi wa wa familia ya kifalme.

## AY ataka heshima isimame

MCHEKESHAJI kutoka Nigeria, Ayo Makun amesema kuna baadhi ya watu wamekuwa wakidharau utu wake.

Baba huyo wa watoto wawili alitumia ukurasa wake wa Instagram, alishiriki katika ujumbe mzito ambao aliutoa kuhusu hali hiyo.

"Nimegundua kuwa ingawa haipendezi machoni pa Mungu kuinua mabega yako juu au kuonyesha tabia ya ubosi, mara nyingi unahitaji kupata heshima unayostahili kutoka kwa wanadamu," isomeka sehemu ya ujumbe huo.



MAKALA



Moja ya hoteli zilizojengwa kwenye fukwe za Bahari ya Hindi, Dar es Salaam. **PICHA: MITANDAO**

# Mgogoro fukwe za Kigamboni mazungumzo yataleta suluhu

**Na Faustine Feliciane**

KUNA wimbo unaousifu uzuri wa nchi hii ukisema, Tanzania yapendeza ina mlima mrefu Kilimanjaro, mabonde na mito ya kuvutia, kadhalika sifa kama hizo zinaiendea Kigamboni moja ya halmashauri za mkoa wa Dar es Salaam zenye fukwe nzuri za Bahari ya Hindi.

Ni uzuri huo unaowavutia wawekezaji kuanzisha miradi ya kuvutia watalii hasa sekta ya hoteli za kitalii za viwango mbalimbali.

Hata hivyo, migogoro ya ardhi kati ya wananchi wa baadhi ya maeneo na wawekezaji imekuwa kero na wakati mwingine kutishia kurudisha nyuma ujenzi wa hoteli katika manispaa hiyo.

Mgogoro ambao unazidi kutia ufa ustawi wa biashara ya hoteli ni ule unahusisha wananchi na wawekezaji ni barabara ya kuingia maeneo ya uwekezaji na uvuvi katika kijiji cha Mikenge kata ya Kimbiji.

Mgogoro huo ambao umedumu kwa muda mrefu na kuepelekea sakata lake kufikishwa mahakamani kwa ajili ya kutatuliwa kisheria.

Mgogoro huo nahusisha mwekezaji kampuni ya ASM (T) LTD, wananchi wa kata ya Kimbiji na wawekezaji wengine wa hoteli zilizopo mbele ya eneo linalomilikiwa kihalali na kampuni hiyo.

Mvutano huo umetokea baada ya mmiliki wa viwanja pacha Kampuni ya ASM, katika kijiji hicho cha Mikenge, kufunga barabara iliyokuwa ikiingia ndani ya eneo la uwekezaji lenye Hotel tatu zilizopo pwani ya bahari ambayo pia wananchi hutumia kwenda katika shughuli zao mbalimbali ikiwamo uvuvi.

Kulingana na wenyeji wa eneo hilo, barabara hiyo ilianza kutumika miaka 30 iliyopita kuingia na kutoka kwenye maeneo ya uvuvi.

Pamoja na Mahakama Kuu kitengo cha Ardhi kutoa hukumu ya kesi ya mgogoro huo na kumpa uhalali mwekezaji ASM, kama mmiliki halali wa viwanja hivyo pacha, bado wananchi na wawekezaji wengine wameiomba Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni kufanya kikao cha pamoja cha kutafuta suluhisho la barabara hiyo.

Mmoja wa wawekezaji katika eneo hilo, Vidate Msoka, anayemiliki Hoteli ya Light House Beach Lodge, amesema licha ya mwenzao kushinda kesi ya mgogoro huo, wanaomba atumie busura kuachia barabara ambayo kwa sasa ameifunga kwa kujenga ukuta.

Anasema, hata katika nakala ya hukumu iliyompa ushindi mwekezaji ASM katika kifungu cha nne mahakama imetoa nafasi ya kuwepo kwa mazungumzo yatakayotoa muafaka wa uwapo wa barabara ya kuingia katika maeneo mingine.

"Sisi kama wawekezaji hatuna shaka na hukumu iliyotolewa na mahakama, lakini tunaomba tu Manispaa ya Kigamboni kama ambavyo sehemu ya hukumu ambayo nakala yake tunayo inavyotoa nafasi ya majadiliano ya kutafuta namna ya kuweka barabara ya kuingia katika maeneo mengine ya wawekezaji," anasema Vidate.

Anasema, kwa upande wao kwa sasa biashara hazifanyiki kutokana na kufungwa kwa barabara hiyo iliyokuwa ikitumiwa kupitisha magari ya wageni wanaokwenda na kutoka kwenye hoteli zilizopo ndani ya eneo hilo.

"Hakuna biashara tunayoifanya kwa sababu ya kutokuwapo kwa barabara ya kuingia kwenye maeneo yetu, lakini tunaendelea kutozwa kodi mbalimbali zikiwamo kodi za Manispaa, tunaoumia ni sisi hivyo uongozi wa Halmashauri ya Kigambo ufanye jitihada za kutatua kero hii, tupo tayari kukaa pamoja kutatua kero hii, halmashauri imeshawishi mwenzetu ASM tukae pamoja kutatua kwa faida ya uchumi wa nchi yetu" anaongeza kusema Vidate.

Kauri hiyo inaungwa mkono na Mwenyekiti wa kijiji cha Mikenge kata hiyo ya Kimbiji, Lameck Mayala alipotafutwa, ambaye anasema wananchi wake wengi katika kijiji hicho ni wavuvi na walikuwa wakitegemea barabara hiyo kingia maeneo ya pwani kwa ajili ya shughuri zao za uvuvi.

Mayala, anasema licha vijana wengi katika kijiji hicho kupoteza kazi walizokuwa wakifanya kwenye hoteli zaidi ya tatu zilizopo katika eneo ambalo kwa sasa halifikiki, pia wananchi wanashindwa kwenda kwenye shughuri zao za kila siku za uvuvi kutokana na changamoto ya barabara rasmi ya kuingia pwani.

"Kabla ya kero hii vijana wetu wengi walipata ajira kwenye hoteli zilizopo mbele ya eneo la ASM, hoteli hizo ziliajiri, lakini kwa sasa hakuna biashara, wengi wameachishwa kazi. Mbaya zaidi tunashindwa kwenda pwani kwa ajili ya shughuri zetu za uvuvi kwa sababu huyu mwekezaji kaziba barabara kwa kujenga ukuta kubwa," anasema Mayala.

Anasema, kwa bahati mbaya mwekezaji ASM hatoi ushrikiano kwao na kwa Halmashauri kila anapoitwa kwa ajili ya kutatua kero hiyo.

"Muda mwingine hata simu akipigiwa hapokei, anapelekewa taarifa ya vikao kupitia kwa wasaidizi wake lakini hatokei, si jambo zuri, wote tupo kwa ajili ya Tanzania yetu, hakuna changamoto isiyokosa suluhisho, tukae kwenye vikao tujadiliane tupate jawabu, sisi shida yetu ni barabara tu ya kutufikisha kwenye maeneo yetu," anasisitiza Mayala.

Kisha akamuomba Mkurugenzi wa halmashauri ambaye suala hili lipo kwenye ofisi yake awasaidie kutatua kwa pamoja kwa njia ya majadiliano na makubaliano.

Mkurugenzi wa kampuni ya ASM (T) LTD, Abdallah Salim Mohamed, kwa upande wake alipotafutiwa kuzungumzia kero hiyo, alitaka kuandikiwa ujumbe mfupi wa maandishi.

"Hilo suala lilishaamuliwa na mahakama, kama kuna jambo lingine niandikie ujumbe," alisema Mohamed alipotafutwa na gazeti hili kupata maoni yake,

Hata hivyo, licha ya kuandikiwa ujumbe mfupi wa maandishi kuombwa kuzungumzia maoni na maombi ya wananchi wa kijiji cha Mikenge na wawekezaji wengine, hakutoa majibu.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kigamboni Erasto Kiwale, alipoulizwa juu ya kero hiyo alikiri mwekezaji ASM kushinda kesi na kwa sasa anafuatilia kuona watatatua vipi kero hiyo.

Anasema, pamoja na ushindi wa mwekezaji huyo bado wananchi na wawekezaji wengine wanahitaji barabara ya kufika kwenye maeno yao na hilo ndilo wanalofanyia kazi kwa sasa.

"Bado tunafanyia kazi suala hili, mimi ni mtendaji na hii ndio kazi yangu, tunafuatilia kuona tunaweka sawa kila kitu, kwa hiyo itoshe kusema bado tunafanyia kazi suala hili, lengo ni kuona kila mmoja anafanya shughuri zake bila vikwazo," alisema Kiwale.

Mkurugenzi huyo alitolea ufafanuzi huo baada ya Mkuu wa Wilaya hiyo, Fatuma Nyangasa kusema jambo hilo lipo kwenye ngazi ya halmashauri.

Kiwale, alisema Halmashauri inataka kuendelea kuifanya Kigamboni kuwa sehemu sahihi ya uwekezaji pia wananchi kuendelea kufanya shughuli zao bila vikwazo vitakavyowarudisha nyuma.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...



Na Adam Fungamwango

# Mkate siha, maziwa KCC yalivyotikisa

## ■Ni kama chips yai tu kwa sasa
## ■Hata zamani watu walitesa

**Na Adam Fungamwango**

KUNA dhana iliyojengeka kuwa zamani watu walipata shida moja kwa moja na hakukuwa na raha hata chembe.

Ni kwa sababu huwa tunasimulia matukio kadhaa ya zamani ambayo yanaonyesha kuna baadhi ya miaka nchi ilikuwa kwenye matatizo.

Wakati mwingine inakuwa ni ya kisiasa na pia kiuchumi. Tumekuwa na makala za unga na mahindi ya njano yaliyotolewa na serikali ya Marekani kwa ajili ya msaada.

Pia, tulikuwa na makala kuhusu aina ya mchele iliyoletwa nchini wakati wa uhaba wa chakula, tukawa na mchele kitumbo, mdundiko, VIP, chereko chereko na aina nyingine nyingi.

Uhaba huu wa chakula na bidhaa mbalimbali ilikuwa ni baada ya vita kati ya Tanzania na Uganda, maarufu kama Vita ya Kagera, ambavyo vilikwenda kumng'oa Nduli Idd Amin Dada.

Ilianza rasmi Oktoba 30, 1978 na kumalizika rasmi 1979, ikiua zaidi ya watu 5,000 kwa pande zote.

Mwanzilishi wa vita hivyo ni Admin aliyedai ardhi ya Kagera ni mali yake akavamia kijeshi.

Rais wa kwanza, Julius Kambarage Nyerere, akiwa ni Amiri Jeshi Mkuu, aliwaongoza vyema wanajeshi 100,000 kumchapa na si kumuondoa kwenye kipande cha ardhi ya Kagera bali pia kumg'oa Uganda na kukimbilia nchini Libya na baadaye Saudi Arabia kabla umauti haujamfika.

Vita ni vita tu, kwani baada ya kumalizika iliiacha nchi ikiwa hoi kiuchumi.

Kama utakumbuka Mwalimu Nyarere, aliilaumu sana OAU, kuwa haikutaka hata kumkemea Amin kutokana na uchokozi wake, hivyo nchi ilivyoingia vitani hakukuwa na msaada wowote kutoka kwenye umoja huo, Tanzania ililazimika kugharamia peke yake vita hiyo, na hata baada ya kumuondoa Nduli Uganda ililazimika kuangalia hali ya usalama nchini humo.

Tanzania, ilitumia rasilimali nyingi kujilinda, ambazo zingezitumiwa kwenye maendeleo kwa ajili ya uchokozi wa Amin.

Ndiyo maana hata vita ilipokwisha kukawa na kauli ya kuwataka kufunga mikanda na kwa haraka haraka wakaona hali inaweza kuwa nzuri baada ya miezi 18 hivi.

Hapo ndipo hali ya uchumi ikaanza kuwa mbaya na kuja kile kipindi cha unga wa Yanga, mchele Kitumbo, chakula kwa Kaya, watu anapanga foleni kwa kuweka matofali na mawe, wapo waliofukuza gari la maiti wakidhani ni gari lililobeba unga, mchele na bidhaa zingine likisambaza kwenye maduka.

Na kuna hadithi nyingi za ukweli na za kutia chumvi zikihusiana na kipindi hicho cha mpito cha hali mbaya ya uchumi.

Hali ilikuwa mbaya kweli, kiasi cha kwamba kulikuwa na uhaba si wa vyakula vikuu tu, bali hata mboga kama maharagwe, sabuni, mafuta ya taa, dawa za mswaki, mbu, na vingine ambavyo ni muhimu kwa mahitaji ya binadamu.

Hiki ndicho kipindi kinachokumbukwa sana na watu wengi waliokuwa watu wazima, vijana au watoto wakati huo.

Lakini kabla ya kuingia kwenye vita nchi ilikuwa kwenye kipindi kizuri na cha raha sana. Kwenye makala zetu huko siku za mbele nitaelekezea sabuni, mafuta na mahaitaji muhimu yaliyokuwa yakipatikana wakati huo.

Kulikuwa na aina nyingi sana za sabuni, mafuta ya kupikia na kupakaa, pamoja na mambo mengi ambayo yaliifanya nchi kuwa kama paradiso.

Inawezekana vijana wa sasa wakaona kwa sasa wao wanafaidi sana na kapata raha kuliko wale wa zamani kwa kuwa na vyakula vizuri na bora, manukato, sabuni na bidhaa mbalimbali za kisasa, wakati mwingine sivyo hivyo.





Wanachowazidi sana sana ni maendeleo ya teknolojia tu kwani kwa sasa imekuwa kubwa sana kiasi cha dunia kuwa kama kijiji tofauti na zamani.

Wakati kwa sasa kuna aina nyingi za mikate ambayo wanaona ni bora sana, lakini sidhani kama inafaikia nusu ya mikate iliyojulikana kwa jina la siha.

Mikate ya siha ndiyo ilikuwa mikate namba moja kwa ubora na bei ya hali ya juu kuliko mingine.

Ndiyo mikate iliyopendwa zaidi na watu walisimama foleni ili kuinunua. Zipo tetesi nyingi zikidai kuwa ilikuwa ngano yake ilikandwa na maziwa pamoja na mayai, baadaye kuokwa. Hakuna uhakika kuhusu hilo, lakini ukweli unabaki pale pale kuwa ni mikate iliyokuwa na ladha tamu na isiyokinahisha.

Kwanza ni laini mno kama sufi ikishika namba moja, huku mikate iliyofuatia kwa ubora ilijulikana kwa jina la gloria.

Wakati huo pia kulikuwa na maziwa maarufu sana wakati huo yakijulikan kama KCC. Vijana wengi wakati huo wakiamka asubuhi, kifungua kinywa chao ilikuwa ni mkate wa siha na maziwa ya KCC.

Pata picha jinsi walivyokuwa wakifaidi. Kwa wale wenye familia, basi ukinunuliwa mkate huo unakwenda kunywa na chai ya maziwa ya KCC basi ilikuwa ni burudani tosha.

Na hapo si kwamba kila familia ilikuwa na uwezo wa kupata kifungua kinywa hicho kila siku. Ni mara chache chache sana, labda siku ambazo mishahara imetoka.

Hata watoto siku wakinywa chai cha maziwa hayo na mkate wa siha ilikuwa ni furaha sana kwao na walitamani kunywa kila siku, lakini haikuwezekana.

Maziwa ya KCC, yakiwa kwenye moto yakitayarishwa kwa ajili ya chai, hata mtu anayepita nje atajua kabisa kuwa ndani chai ya maziwa inapikwa kutokana na harufu yake ya kuvutia.

Mikate ya siha ilitengenezwa na Shirikika la Usagaji la Taifa (NMC), ambapo mkate huo ulikuwa ni moja kati ya bidhaa zake kubwa na maarufu.

Kwa bahti mbaya badaye ilianza kupoteza ubora kwa sababu ambazo hazikueleweka vyema, na baadaye ikafuatia kuyumba kwa kampuni hiyo kama ambayo nyingi zilivyoanza kuterereka kwa kushindwa kujiendesha kutokana na sababu mbalimbali, ikiwamo athari ya Vita vya Kagera, pia hata ubadhirifu.

**Tuma meseji 0716 350534**

# Kenya yasubiri uamuzi wa mahakama kuhusu ushindi wa William Ruto

**NAIROTI,** KENYA

MAHAKAMA ya Juu nchini Kenya ilihitimisha vikao vyake jana Ijumaa baada ya kusikiliza hoja za wanaopinga na kuunga mkono kesi ya matokeo ya uchaguzi mkuu wa Rais uliofanyika Agosti 9.

Jopo la majaji saba litapata nafasi kutathmini yaliyosemwa na kutoa uamuzi wao Jumatatu ijayo. Mawakili wa pande zote ili wanajibu maswali ya majaji baada ya kuwasilisha hoja zao.

Kwenye kikao cha mwisho, wakili wa Azimio la Umoja One Kenya, Julie Soweto, aliielezea mahakama kuwa raia wa Venezuela Jose Camargo ndiye aliyeamua atakayekuwa rais wa Kenya.

Dhamira ya wakili Julie Soweto ilikuwa kuionyesha mahakama jinsi matokeo ya uchaguzi wa rais yalivyochakachuliwa kwenye mtandao wa Tume ya Uchaguzi, IEBC.

Raia huyo wa kigeni ni mmoja wa wale wa Venezuela waliokamatwa kwenye uwanja wa ndege wa kimataifa wa JKIA kwa madai ya kuwa na mkono kuvuruga uchaguzi.

Camargo alikamatwa pamoja na Joel Gustavo Rodriguez Garcia na Salavador Javier Suarez tarehe 21 mwezi wa Julai wakiwa na vifaa vya uchaguzi. Inasadikika walikuwa wafanyakazi wa kampuni ya teknolojia ya uchaguzi ya Smartmatic International.

Kabla ya wakili Julie Soweto kujieleza mbele ya mahakama, Paul Mwangi, alisisitiza kuwa Camargo aliacha alama za video vyake kwenye fomu hizo.

Tume ya uchaguzi yapinga madai ya upande wa walalamikaji

Kwa upande mwingine, mawakili wa tume ya uchaguzi na mipaka wamekanusha madai hayo ya upande wa walalamikaji ya mkono wa raia huyo wa Venezuela kwenye uchaguzi wa rais.


Kulingana na wakili Mahat Somane, watatu hao walipewa nafasi maalum ya kuingia kwenye seva hiyo basi hawakuwa na uwezo wa kusababisha hila.

Wakili Somane aliwakilisha tume ya uchaguzi ya IEBC.

Kadhalika tume ya uchaguzi imejitetea mintarafu tofauti ya idadi ya kura ya rais na nyadhifa nyengine ukizingatia karatasi zilizotumika vibaya.

Jana ni siku ya kuhitimisha vikao vya kesi ya kupinga matokeo ya uchaguzi wa rais wa Agosti 9 yaliyompa ushindi rais mteule William Ruto.

Jopo la majaji saba wa Mahakama ya Juu linatarajiwa kuitoa kauli yake Jumatatu ijayo.



Mwenyekiti wa IEBC, Wafula Chebukati. **PICHA:MTANDAO**

### ODINGA MACHO KWENYE RUNINGA MAWAKILI WAKIMTETEA

Mawakili wa mgombea aliyeshindwa katika uchaguzi wa urais wa Agosti 9 nchini Kenya wanaunga mkono ombi lake la kupinga matokeo katika Mahakama ya Juu katika mji mkuu, Nairobi.

Walionyesha kanda za video zinazodai kuwa fomu za matokeo zilibadilishwa ili kumpendelea rais mteule William Ruto.

Lakini madai haya yalikanushwa na mawakili wa Tume ya Uchaguzi na wale wa Ruto.

Majaji saba wa Mahakama ya Juu watamaliza kusikiliza kesi ili kuandika hukumu ambayo itatolewa wiki ijayo Jumatatu.

Akaunti rasmi ya Twitter ya Odinga imeshirikisha mtandaoni picha ya mwanasiasa huyo mkongwe wa Kenya akifuatilia shughuli za mahakama kwenye runinga.

Iwapo Chebukati atashtakiwa, Uhuru ataendelea kuhudumu hadi Rais mpya aapishwe

Wakili Willis Otieno alijibu maswali ya Mahakama ya Juu kuhusu iwapo kutakuwa na pengo iwapo mahakama ya juu itaamua kumfungulia mashtaka Mwenyekiti wa Tume Huru ya Uchaguzi na Mipaka (IEBC), Wafula Chebukati.

Kulingana na Otieno, Kifungu cha 142 cha Katiba kinasema kuwa Rais ambaye yuko madarakani anaendelea hadi atakapochaguliwa mpya.

"Rais atashika madaraka yake kwa muhula unaoanza tarehe ambayo Rais aliapishwa, na kumalizika wakati mtu anayefuata aliyechaguliwa kuwa Rais kwa mujibu wa Ibara ya 136 (2) (a) anapoapishwa," ibara ya 142 ya Katiba inasema.

Kwa hakika, Katiba katika 142 (2) inaongeza kuwa mtu hatashika madaraka ya Rais kwa zaidi ya mihula miwili.

Otieno alishikilia kuwa Chebukati hajazuiliwa kufa na anaweza kujiuzulu lakini hii haimaanishi kuwa Tume na uchaguzi bado hautaendeshwa nchini.

"Mahakama hii haifai kukwepa iwapo itaona inafaa kumfungulia mashtaka Mwenyekiti Chebukati kwa makosa na njia ya pekee ambayo ameshughulikia uchaguzi kwa madhara ya Wakenya," aliongezea.

### WAKILI WA RAILA AONYESHA FOMU KATIKA SEVA YA IEBC

Wakili wa Raila aonyesha fomu katika seva ya IEBC iliyo na jina la raia wa Venezuela.

Wakili wa mlalamishi Raila Odinga katika kesi inayopinga uchaguzi wa Rais Mteule William Ruto katika mahakama ya Juu Julie Soweto alionyesha moja kwa moja kanda ya video iliyoonyesha hitilafu kutoka kwa tovuti ya tume ya uchaguzi nchini Kenya IEBC.

Wakati wa kusikilizwa kwa kesi ya kupinga uchaguzi wa urais, alitoa fomu katika tovuti hiyo kutoka Shule ya Msingi ya Gacharaigo katika Kaunti ya Murang'a iliyokuwa na jina la raia wa Venezuela Jose Camargo.

"Mahali nilipo muhuri wa IEBC unaonekana umepachikwa juu ya muhuri mwingine. Tumeombwa tuonyeshe jinsi takwimu zinavyobadilishwa. Tukiangalia kura zilizopigwa, nambari ya kwanza ni ya Raila Odinga aliyepata 55, Ruto 260, Mwaure 1 na Wajackoyah 0.

Iwapo tutajumlisha jumla ya kura zilizopigwa tutapata 316. Jumla ya kura zote zilizopigwa katika fomu hiyo ni 321, ikiwa ni tofauti na kile tulichoona.

Hii ikimaanisha kwamba tayari hesabu hiyo ina makosa," alisema.

"Tuliambiwa na wakili wa IEBC Eric Gumbo kwamba hakukuwapo raia wa kigeni katika uchaguzi huu. Tuliambiwa kwamba hawakuweza kuingilia seva za IEBC .

Tazama Juu kushoto katika fomu hii kuna jina la Jose Camargo. Huyu ndiye mtu aliyefanya maamuzi ya uchaguzi huu. Je jina hili liliingiaje hapa?" , aliuliza.

Soweto alihoji kwamba bwana Carmago ndiye aliyekuwa akiingilia fomu zote 34ª katika seva ya tume ya Uchaguzi ya IEBC.

"Ishara ya kuingilia fomu hizi iliachwa. Kwa Neema ya Mungu , tulipata kitu . Hili hatukujifanyia. Hivi ndivyo mambo yalivyofanyika."

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**SUZANA EMMANUEL MAPUNDA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S/4355/0043** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **MAENDELEO SECONDARY SCHOOL** mwaka **2013.** Kwa yeytote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DAR/URA/RB/323057/2022**

**Summons to appear (O.VR.20 (1) of (CPC)**
**(Substituted Service)**
**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(LAND DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**
**LAND CASE NO. 82 OF 2022**
**CHACHA MANTAGE......APPLICANT**
**VERSUS**
**FLAVIAN MATHEW NYENDIKUU & ANOTHER ...............RESPONDENTS**

**TO: MZIGE AUCTION MART,**
**MBAGALA TOANGOMA,**
**SHAURI MOYO STREET,**
**DAR ES SALAAM.**

**WHEREAS:** The above named **APPLICANT** has instituted an **APPLICATION** against you, you are hereby summoned to appear in this court in person or by advocate or authorized Agent on **22 day of SEPTEMBER, 2022** at 09:00am before **Hon. A. MSAFIRI, JUDGE (Chamber No. 3)** in the morning to answer the said **APPLICATION** and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

**TAKE NOTICE** that, in default of your appearance on that day the said Application will be heard and determined in your absence.

**Given under my hand and the seal of this Court, this 31 day of August, 2022.**

DEPUTY REGISTRAR

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya**
**DODOMA MJINI**
**Kituo Cha CHAMWINO**
**Usimamizi wa Mirathi Na 47/2022 Mkoa Dodoma**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU**
**SALMA .J. CHUWA WA CHAMWINO MJINI**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALITOLEWA NA RUKIA CHARISE MABERE**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo Mnamo tarehe 03 Mwezi 10 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa Msimamizi wa mirathi hiyo .

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.

* Marehemu hakuacha wosia
* Futa isiyohusika

**Imetolewa Leo Tarehe 01 Mwezi 09 Mwaka 2022**

HAKIMU
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
CHAMWINO-MJINI
DODOMA

## KUPOTEA KWA CHETI



**REVOCATUS .K. MILLAMBO** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0146-0027** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **NYEGEZI SEMINARY** mwaka **2008 .** kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA : UD/RB/3922/2016**

## KUPOTEA KWA CHETI



**IRENE JORAM MASUKI** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0224-0031** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **KIFUNGILO GIRLS SEKONDARI** mwaka **2014.** Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha Polisi.

**Taarifa ya Polisi: DAR/MSI/RB/345686/2022.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ALEX EXAVERY CHODOTA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA yenye** namba za usajili **T 740 DVM LENYE CHASES NAMBA: GRS 1800051525 ENGINE NO :4GR0237382** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa polisi

**Taarifa ya polisi RB. Namba IRI/IRI/RB/336558/2022**

## ANATAFUTWA



2170278

Ndugu **Shamte Abeid Mohamed** mwenye Pasipoti **No AB585606** anaendelea kutafutwa na familia yake ikishirikiana na jeshi la polisi kwa tuhuma za kujihusisha na vitendo vya kinyume na maadili. Yeyote atakae muona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu nae. Zawadi nono itatolewa kwa yeyote atakayempata

**POLISI TAARIFA ni UBUNG/RB/174/22**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676***

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTRIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 0782253676**




**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MGENI wa ajabu atatokea kwenye kijiji cha Semwanza, Lugoba mkoani Pwani. Anakotoka hakujulikani. Watu wote wanamwogopa. Ni kwa sababu hawamjui. Msichana Siwatu anajitolea kumsaidia mgeni huyo. Kwa kufanya hivyo, anabezwa kwa maneno mengi ya kejeli kwa kumsaidia mtu asiyemjua ambaye anaweza kuwa hatari katika kijiji. Baadhi ya viongozi wa kijiji waliungana na wanakijiji kutaka wamtimue mgeni hiyo asiyejulikana, lakini akakataa katakata. Pamoja na kutishwa kuwa atatengwa na kijiji, bado msichana huyo alisimama na msimamo wake ule ule wa kumsaidia kwa sababu alikuwa na shida kubwa.

Matokeo haya, yanamuingiza Siwatu kwenye msukosuko mkubwa ambao hajawahi kuupata kwenye maisha yake kiasi cha kumkatisha tamaa. Fuatilia kisa hiki.

# Kama ipo, ipo tu-21

**Na Adam Fungamwango, (0716 350534)**




Kwa muda mrefu nimeishi kwa baba na mama bila ya kuwa na mpenzi. Baba na mama alitaka sana kuniozosha, lakini nilikataa.

Kuna wakati wazazi wangu walitaka kujidhihirisha kama nina tatizo la kiafya kwa sababu hawakuwahi hata siku moja kuniona na mwanamke. Walipojidhihirisha wakaniacha kama nilivyo. Bahati mbaya baba yangu alifariki. Nasikitika amefariki kabla ya kukuoa wewe.

Muda wote huo kwa kweli niliona wanawake wengi sana, na wengine walinitamkia wenyewe tu kama wananipenda na wengine wakitaka niwaoe, lakini nilikataa. Sikuona hata mmoja ambaye ananifaa.

Lakini kwako nimefika kikomo. Nimetokea kukupenda sana. Utajiuliza kwa nini? Hao uliwaona na kwa nini wewe sijakuona na nimetokea kukupenda na moja kwa moja nataka nikuoe? Haya nitakuja kukwambia ana kwa ana tukikutana." Barua iliendelea kumfikirisha Siwatu. Alijiuliza ni kwa nini mchumba huyo aandike maneno yale wakati anakuja yeye mwenyewe jioni?

Hakupata jibu. Labda atakuja kumuuliza jioni hiyo akija. Akaendelea.

"Kwa sasa nimebaki na mama yangu na dada zangu wawili ambao wote wameolewa. Walikuwa wanalia siku zote nipate mke. Sasa watafurahi kwa sababu nitakwenda kumuoa mwanamke wa ndoto zangu. Mwanamke ambaye nina uhakika tutaishi milele mpaka kufa. Nina uhakika na hilo."

Uandishi wa mchumba wake huyo ulimshangaza sana Siwatu. Ni kwa sababu alionyesha iliandikwa na mtu anayejiamini na anayeonekana kama vile ana uhakika na anachokifanya. Pia hana wasiwasi kama atamkosa mchumba.

"Anachekesha huyu, yaani mpaka sasa kashajiaminisha kuwa mimi ni mke wake. Haya bana, enhee." Akajisemesha mwenyewe akionekana kuvutiwa kidogo na maelezo hayo. Akaendelea kuisoma barua hiyo ambapo pamoja na kwamba imeandikwa na mtu ambaye hamfahamu, alimkubali kabla hajamuona, lakini kwa sasa amemtumbukia nyongo baada ta ujio wa Bakari, lakini stori yake na uandishi wake ulimfurahisha. Akajikuta badala ya machozi kumtoka kama ilivyokuwa mwanzo, akaanza kutabasamu na kuwa na shauku ya kuendelea kuisoma.

"Hapa nafikiria jinsi harusi yetu itakavyokuwa ya kufana sana. Kila mtu atafurahi sana kwa kumpata mtu aliyempenda toka kwenye uvungu wa moyo wake..." Alipofika hapa akaangua kicheko. Ni muda si mrefu alikuwa anatokwa machozi.

"Yaani huyu kaka jamani looh, kanishinda tabia. Hebu aje jioni nimuone." Akajisemea akimalizika na tabasamu.

"Samahani sikuweza kuja wiki iliyopita kwa sababu kuna mkasa mkubwa ulinipata.

Nilikiwa kwenye shughuli zangu za biashara, nilitekwa na watu waliopiga risasi juu kuniamuru nisimame. Nilipaki Ranger Rover yangu, haraka haraka wakaingia ndani ya gari. Nia yao ilikuwa ni kuniua na waliniambia kabisa kuwa wametumwa na mmoja wa mfanyabiashara mwenzangu. Wakaniambia wamechukua pesa ili waniue.

Sikuwa tena na matumaini ya kuishi. Niliwaza vitu vingi. Niliwaza dada zangu watakapokuwa wanamtafuta. Nikamuwaza mama yangu jinsi atakapokuwa anawahimiza mabinti zake kunitafuta.

Nikawaza jinsi dada zangu watakapopata ugumu kuipata maiti yangu, kiukweli nilikufa moyo kabisa. Kwa bahati nzuri leo hii niko hai. Kwa nini niko hai? Kitu gani kimetokea hadi jamaa wakaahindwa kukamilisha misheni yao, nitakuja kukwambia mwenyewe kwa mdomo wangu jioni nitakapofika hapo mpenzi wangu." Karatasi sita zilizoandikwa zikawa zimemalizika.

**"Ndicho ulichokuwa unasoma hiki?" Akauliza huku akitabasamu. Siwatu hakujibu, kwani hakujua kama ni tabasamu halisi au la bandia.**

Wakati akiwaza yaliyoandikwa, mlango uligongwa na Bakari aliingia.

Siwatu hakutaka kabisa Bakari ajue kama alikuwa anasoma barua. Akajua kama akigundua ni ya huyo mwanaume aliyemtolea mahari, anaweza kukasirika.

Akataka kuificha karatasi ile. Bakari aliiona. Hakuonyesha hisia yoyote kama kuna kitu anataka kufanya. Akamsogelea. Ghafla akamnyang'anya. Siwatu alishtuka, lakini hakuwa na la kufanya.

"Nataka nisome huyu mjinga anasemaje?" Siwatu alikaa pembeni akiwa na wasiwasi mkubwa juu ya tukio hilo.

Bakari alisoma kila kitu, akamaliza. Cha ajabu, alichokuwa anafikiria Siwatu siyo kilichotokea.

Akidhani atakasairika kutokana na barua hiyo, badala yake akatasamu.

"Ndicho ulichokuwa unasoma hiki?" Akauliza huku akitabasamu. Siwatu hakujibu, kwani hakujua kama ni tabasamu halisi au la bandia.

"Jamaa ni mwandishi mzuri sana huyu. Hata mimi kanifurahisha. Sasa kama anajifanya anatumia umahiri wake wa kuandika kukushawishi wewe, mimi nitatumia mdomo."

Bado Siwatu alikuwa njia panda. Hakuelewa Bakari alikuwa anataka kufanya nini.

"Hii stori yake sijui ya ukweli au ya uongo, mimi nitakuelezea yangu kwa mdomo."

"Unafanyaje? Mbona una masihara sana Bakari ?"

"Na mimi nina yangu, ila yeye kaandika, mimi nitakuhadithia kwa mdomo."

"Hadi anakuja hapa saa 12:00 jioni nitakuwa nimeshamaliza. Na yeye nitakuwa nishammaliza kabisa."

"Bakari kuna vitu vingine siyo vya masihara bwana, nini kwani, yeye si kaleta tu karatasi kwani ndiyo nimesema amefanikiwa?"

"Hapana, huyu amedhamiria, na nikifanya masihara hapa nitatoka kapa. Naona kabisa dalili za kukukosa. Hebu njoo hapa tukae nikupe ya kwangu halafu upime mwenyewe stori ipi ni nzuri zaidi ya nyingine."

Bado Siwatu alikuwa hajamuelewa au kujua nia ya Bakari ni nini. Hata hivyo moyo ulitulia baada ya kuona hajakasirika kumkuta na barua ile, na hata baada ya kuisoma.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# AFRICARRIERS YAIPA SIMBA QUEENS BASI LA KISASA

**Na Saada Akida**

KAMPUNI ya Africarriers ya hapa nchini imewakabidhi basi la kisasa mabingwa wa soka la wanawake wa Afrika Mashariki na Kati, Simba Queens basi lenye thamani ya Sh. milioni 100.1.

Simba Queens, ambao pia ni mabingwa wa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania, wameweka rekodi kuwa timu ya kwanza ya wanawake kumiliki basi lake badala ya kuazimwa magari yanayotumiwa na klabu za wanaume.

Mkuu wa Rasirimali Watu wa Africarriers, Lydia George, alisema kampuni hiyo imeamua kutoa basi hilo kutokana na mafanikio ambayo Simba Queens imeyapata tangu katika mashindano ya ndani na ya kimataifa.

Lydia, alisema awali waliingia udhamini na Simba, lakini uongozi wa kampuni hiyo umeona pia uwekeze katika timu hiyo ya wanawake na sasa wanafurahia matunda yanayopatikana.

"Awali tuliingia udhamini na timu ya wanaume na hivi leo tumeingia makubaliano na Simba kwa kuwadhamini usafiri Simba Queens, kwa kuwakabidhi basi," alisema Lydia.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, alisema wanafurahi kuona Africarriers walihitaji kuidhamini Simba sasa wameingia katika udhamini wa timu ya wanawake.

Barbara, alisema kufanya vizuri kwa Simba Queens ambayo imetwaa ubingwa Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania mara tatu mfululizo na kubeba Kombe la CECAFA, kumeishawishi kampuni hiyo kuingia udhamini.

"Leo tumeingia mkataba na Africarriers kwa Simba Queens, ni klabu ya kwanza ya wanawake kuwa na basi lake, hii kwa sababu ya mafanikio tunayoendelea kupata, kwa sasa timu yetu hiyo itaenda kuwakilisha CECAFA katika fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake," alisema Barbara.

Aliongeza ana imani udhamini huo utaleta chachu kwa makampuni mengine lakini klabu ikiendelea kufanya mazungumzo na Africarriers kukubali kuwa wadhamini wakuu wa timu hiyo.

Kocha Mkuu wa Simba Queens, Sebastian Nkoma, alisema kwa sasa timu yao inaendelea na maandalizi kwa ajili ya kuelekea katika fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika ambapo zitafanyika Morocco baadaye mwaka huu.

Nkoma, alisema kikosi chake huenda kikaenda kuweka kambi nje ya nchi huku taarifa za ndani zikieleza maandalizi yameanza ya kuwapeleka Dubai.




Mkurugenzi wa Masoko wa Kampuni ya M-Bet Tanzania, Allen Mushi (kushoto) akimkabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 113.7, Raphael Daudi (katikati), baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 za ligi mbalimbali duniani kupitia mchezo wa Perfect 12, unaondeshwa na kampuni hiyo. Kulia ni Mkuu wa Kitengo Cha Wateja Binafsi wa Benki ya CRDB, Stephen Adili. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shabiki Simba achekelea M-BET

**Na Mwandishi Wetu**

SHABIKI wa Simba wa jijini, Dar es Salaam, Raphael Daudi, ameshinda kitita cha Sh. milioni 113.7 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 12 za mchezo wa Perfect 12 unaondeshwa na Kampuni ya M-Bet Tanzania.

Daudi ambaye ni muuza duka eneo la Ubungo Riverside alisema haikuwa kazi rahisi kwa yeye kushinda kiasi kikubwa cha fedha hicho kutokana na ugumu wa kubashiri kwa baadhi ya timu zilizokuwa zinacheza ikiwamo mechi kati ya Crystal Palace dhidi ya Brentford FC kutokana na matokeo ya timu zote mbili kabla ya mchezo huo.

Daudi, ambaye pia ni shabiki wa klabu ya Simba alisema kuwa atazitumia fedha hizo kwa kuongeza mtaji katika biashara zake na nyingine kujiendeleza kimasomo.

Mkurugenzi wa Masoko wa M-Bet Tanzania, Allen Mushi alisema Daudi anakuwa mshindi wa nane wa Jackpot ya PERFECT 12 tangu kuanza kwa mwaka huu.

Mkuu wa Kitengo Cha Wateja Binafsi wa Benki CRDB, Stephen Adili, alimpongeza Daudi kwa kushinda kiasi kikubwa cha fedha na kumshauri kutumia kiasi hicho cha fedha kuwekeza.

"Nampongeza Daudi kwa ushindi huu mkubwa na kikubwa zaidi ni mteja wa benki yetu yenye ushirikiano mkubwa na kampuni ya M-Bet Tanzania. Nawaomba vijana wenye umri kuanzia miaka 18 kubashiri na M-BET na vile vile kuweka fedha zao katika benki yetu ili kushiriki katika promosheni yetu maarufu ya kuelekea Kombe la Dunia nchini Qatar," alisema Adili.

## Timu za majeshi Afrika kibaruani

**Na Saada Akida**

MASHINDANO ya Majeshi ya Polisi katika Ukanda wa Kusini mwa Afrika (SARPPCO) yanatarajiwa kuanza leo hadi Septemba 16, mwaka huu kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Mratibu Msaidizi wa mashindano hayo nchini, ACP, Hashim Abdallah, alisema maandalizi yanaendelea vizuri na timu zote zilizothibitisha kushiriki michuano hiyo zimewasili.

"Tumejipanga vizuri kuelekea mashindano haya ikiwamo sehemu za kufikia timu, kwa upande wetu Tanzania timu zote zinazoshiriki michezo hii ziko tayari kufanya vizuri," alisema Hashim.

Alitaja nchi ambazo zitachuana katika mashindano hayo ni pamoja na Malawi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Angola, Afrika ya Kusini, Zimbabwe na wenyeji Tanzania.

Alitaja michezo itakayoshindaniwa ni soka kwa wanawake na wanaume, netiboli, riadha, cheese, darts, wavu na kikapu kwa wanawake na Wanaume.

## Klabu za vishale kuchuana Uganda

**Na Shufaa Lyimo**

MASHINDANO ya wazi ya mchezo wa vishali Afrika Mashariki yamepangwa kufanyika kuanzia Septemba 24 hadi 26, mwaka huu jijini Kampala, Uganda.

Makamu Mwenyekiti wa Chama cha Vishale Tanzania (TADA), Redemta Mwebesa, alisema mashindano hayo yatashirikisha nchi tatu ambazo ni Kenya, Tanzania na wenyeji Uganda.

**"Maandalizi kuelekea mashindano hayo ya naendelea vizuri, vilabu vyote na timu za mikoa zinaruhusiwa kushiriki," alisema Mwebesa.**

Kiongozi huyo alizitaka klabu za hapa nchini kujitokeza kwa wingi kushiriki michuano hiyo kama sehemu ya kutangaza vipaji vyao katika ngazi ya kimataifa.

"Mchezo huu unazidi kushika kasi tofauti na ilivyokuwa miaka iliyopita, ninaomba Watanzania wasichoke kutupa ushirikiano kama wanavyofanya kwenye mchezo wa soka," Mwebesa alisema.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**RONALDO, NAPOLI WALIKWAMA**

MKURUGENZI wa Napoli, Cristiano Giuntoli, amesema "hakukuwa na makubaliano thabiti" kati ya klabu hiyo ya Serie A na mshambuliaji wa Manchester United na Ureno, Cristiano Ronaldo mwenye umri wa miaka 37. ***(DAZN, via Manchester Evening News)***

**BAYERN YAMTAJA RONALDO**

MKURUGENZI wa Michezo wa Bayern Munich, Hasan Salihamidzic, amesema Cristiano Ronaldo hakuwa chaguo kwao msimu huu wa joto kwani "walikuwa wakifanya mambo mengine".***(Sky Sports)***

**VILLA YAMGOMEA LUIZ**

KLABU ya Aston Villa ilikataa ofa tatu, ikiwa ni pamoja na ofa ya mwisho ya pauni milioni 25, kutoka kwa Arsenal kwa ajili ya kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Brazil, Douglas Luiz mwenye umri wa miaka 24. ***(Sky Sports)***

**PEDRO AIKUBALI WATFORD**

MSHAMBULIAJI wa Watford, Joao Pedro, amesema "amejitolea kikamilifu kwa klabu" baada ya kukataa ofa kutoka kwa Everton kwa ajili ya Mbrazil huyo mwenye umri wa miaka 20.***(Watford Observer)***

**WATFORD: SARR HAONDOKI**

KLABU ya Watford ilisimama kidete kuhakikisha inambakisha winga wa Timu ya Taifa ya Senegal, Ismaila Sarr, mwenye umri wa miaka 24, licha ya kupokea ofa ya pauni milioni 25 kutoka kwa Aston Villa na Crystal Palace. ***(Athletic)***

**AJAX YAIBANIA CHELSEA**

KLABU ya Ajax iliizuia Chelsea kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Mexico, Edson Alvarez mwenye umri wa miaka 24, kwa sababu klabu hiyo ya Uholanzi ilihisi imepoteza wachezaji wengi msimu huu. ***(De Telegraaf, via Mail)***

**AOUAR ABAKISHWA FULHAM**

KIUNGO wa kati wa Lyon na Timu ya Taifa ya Ufaransa, Houssem Aouar mwenye umri wa miaka 24, atasalia katika klabu hiyo, licha ya kufikia makubaliano ya kujiunga na Nottingham Forest na kuwa na nia ya kuondoka Fulham. ***(L'Equipe)***

**MILAN YAMKATAA LEAO**

AC Milan ilikataa ombi la Chelsea la euro milioni 80 pamoja na mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ureno, Rafael Leao mwenye umri wa miaka 23. ***(Duncan Castles)***

**MARTINELL ALIKARIBIA ARSENAL**

KLABU ya Arsenal ilikuwa ikijiandaa kupigania kumnunua mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Brazil, Gabriel Martinelli kutoka AC Milan, ambaye ilimwona mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21 kama mbadala wa Leao. ***(Calciomercato)***

**DIAZ KUONDOKA JANUARI**

BLACKBURN Rovers itazingatia ofa za kabla ya mkataba wa awali kwa mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Chile, Ben Brereton Diaz, mwenye miaka 23 Januari baada ya klabu hiyo kukataa ombi la pauni milioni 12 kutoka kwa Fulham na Everton. ***(Telegraph)***

**PSG KUMFUATA SKRINIAR**

KLABU ya Paris St-Germain imeachana na jaribio lao la kumsajili beki wa Slovakia kutoka Inter Milan, Milan Skriniar msimu huu, lakini wanaweza kurejea katika harakati zao za kumnasa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 katika dirisha la usajili la Januari. ***(L'Equipe)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# AUBAMEYANG RASMI ASAJILIWA NA CHELSEA

●●● Asaini mkataba wa miaka miwili na The Blues baada ya kuona hana nafasi...

**LONDON, England**

KLABU ya Chelsea imekamilisha usajili wa mshambuliaji, Pierre- Emerick Aubameyang kutoka Barcelona kwa dau la pauni milioni 10.3.

Aubameyang ambaye alikuwa ni mshambuliaji wa zamani wa Arsenal amesaini mkataba wa miaka miwili wa kuitumikia Chelsea.

Mchezaji huyo alijiunga na Barcelona ya Kocha, Xhavi Hernandez, msimu uliopita ambapo alianza vizuri klabuni hapo.

Lakini baada ya usajili wa Roberto Lewandowski na uhaba wa fedha ambao Barcelona wanao waliamuaa kumuuza kwa sababu wameshapata mshambuliaji wa daraja la juu.

Aubameyang ambaye ni raia wa Gabon mwenye umri wa miaka 33 anaenda kuungana na vijana wa darajani.

Chelsea kwa misimu miwili iliyopita walimsajili mshambuliaji, Romelu Lukaku kutoka Inter Milan ambaye hakufanikiwa sana na kumrudisha kwa mkopo huko Italia.

Pia wamemtoa kwa mkopo, Timo Werner kwenda RB ya Ujerumani.

Chelsea imeanza msimu huu wa kusuasua kutokana na kukosa watu sahihi kwenye muda sahihi wakipoteza nafasi za wazi za kufunga mabao.

The Blues hao sasa wamemleta mshambuliaji huyo ambaye aliwahi kuchukua kiatu cha ufungaji bora katika Ligi Kuu England, ili kuongeza nguvu.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,027,3

MECHI KALI
CHELSEA
VERSUS
WEST HAM
1 | 1.49
X | 4.31
2 | 5.61

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa airtel money ZANTEL EZYPESA
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# BRUNO AWASHUKURU MASHABIKI WA UNITED

**LONDON, England**

KIUNGO mshambuliaji wa Manchester United, Bruno Fernandez, amewashukuru mashabiki wao kwa kusafiri mpaka katika mji wa Leicester kwa ajili ya kuwapa ushirikiano wa kushangilia.

Bruno kupitia ukurasa wake wa Twitter ameposti ujumbe uliosomeka; "Alama tatu nyingine tukiwa ugenini, shukrani nyingi na za pekee kwa mashabiki waliosafiri nasi mpaka Leicester wenye hali ya hewa nzuri, sasa ni muda wa kuimarika na kurejea tena siku ya Jumapili."

Manchester United walikuwa ugenini dhidi ya Leicester City ambapo walipata ushindi mgumu wa bao 1-0, bao hilo pekee likifungwa na Jardon Sancho aliyepokea pasi mujarabu kutoka kwa Marcus Rashford dakika ya 23, goli lililodumu mpaka filimbi ya mwisho ya mwamuzi, juzi Alhamisi usiku.

Ushindi huo unakuwa ni wa tatu mfululizo kwa Manchester United baada ya kushinda dhidi ya Liverpool, wakashinda tena mbele ya Southampton na huo ukakamilisha rekodi ya ushindi katika mechi tatu mfululizo.

Mchezo unaofuata watakutana na Arsenal waliopo nafasi ya kwanza katika msimamo wa Ligi Kuu England ambao hawajapoteza mechi hata moja.




# Lukaku kuwakosa AC Milan

**MILAN, Italia**

MSHAMBULIAJI wa Inter Milan, Romelu Lukaku yuko shakani kukosa mechi ya watani wa jadi itakayochezwa wikiendi hii kutokana na majeraha aliyonayo.

Lukaku aliondolewa katika kikosi cha Inter Milan ambacho kilicheza na Cremonese katika ya wiki hii kutokana na kupata majeraha ya nyonga.

Lukaku alipata majeraha hayo katika mazoezi baada ya kikosi hicho kutoka kwenye kipigo cha mabao 3-0 dhidi ya Lazio, mechi iliyochezwa Ijumaa iliyopita.

Pia Lukaku anatarajia kukosa mchezo wa ufunguzi wa Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Bayern Munich utakaochezwa katikati ya wiki ijayo.

Hizi ni habari mbaya kwa Kocha, Simone Inzaghi, ambaye anataka kuuwasha tena moto wa safu hiyo ya ushambulliaji kwa kuwaunganisha tena Lukaku na Lautaro Martinez.



HABARI MICHEZO


393,141/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 03/09/22 | 17:00 | Swansea City vs Queens Park Rangers | 2.33 | 3.20 | 2.95 |
| 02. 03/09/22 | 17:00 | Rotherham United vs Watford FC | 2.90 | 3.15 | 2.41 |
| 03. 03/09/22 | 19:00 | AC Milan vs Inter Milano | 2.60 | 3.25 | 2.60 |
| 04. 03/09/22 | 19:00 | FC Sion vs FC Basel 1893 | 2.60 | 3.30 | 2.50 |
| 05. 03/09/22 | 19:30 | Real Sociedad San Sebastian vs Atletico Madrid | 2.80 | 3.10 | 2.50 |
| 06. 03/09/22 | 19:30 | SD Ponferradina vs Sporting Gijon | 2.55 | 3.20 | 2.65 |
| 07. 03/09/22 | 20:00 | AC Omonia Nicosia vs AEK Larnaca | 2.50 | 3.35 | 2.60 |
| 08. 03/09/22 | 21:45 | Lazio Rome vs SSC Napoli | 2.80 | 3.35 | 2.36 |
| 09. 04/09/22 | 02:00 | New York Red Bulls vs Philadelphia Union | 2.35 | 3.45 | 2.75 |
| 10. 04/09/22 | 14:00 | Reading FC vs Stoke City | 2.85 | 3.15 | 2.43 |
| 11. 04/09/22 | 14:30 | Hansa Rostock vs Hannover 96 | 2.49 | 3.35 | 2.65 |
| 12. 04/09/22 | 15:00 | Odense Boldklub vs Viborg FF | 2.55 | 3.50 | 2.48 |
| 13. 04/09/22 | 16:00 | AC Ajaccio vs FC Lorient | 2.37 | 3.25 | 2.85 |
| 14. 04/09/22 | 16:00 | Stade Brest 29 vs Strasbourg Alsace | 2.90 | 3.40 | 2.28 |
| 15. 04/09/22 | 17:00 | Huddersfield Town vs Blackpool | 2.55 | 3.15 | 2.70 |
| 16. 04/09/22 | 18:30 | Manchester United vs Arsenal FC | 2.41 | 3.45 | 2.65 |
| 17. 04/09/22 | 21:30 | Aris Thessaloniki vs PAOK Thessaloniki | 2.39 | 3.15 | 2.90 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 03/09/2022

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 1511 | Celtic vs Rangers | 1.88 | 3.61 | 3.76 |
| 14:30 | 1950 | Everton vs Liverpool | 6.62 | 4.72 | 1.39 |
| 15:00 | 4384 | Mallorca vs Girona | 2.15 | 3.13 | 3.49 |
| 15:00 | 5494 | Alaves vs Las Palmas UD | 2.24 | 3.06 | 3.26 |
| 16:00 | 1729 | Moreirense vs Oliveirense | 1.46 | 4.18 | 6.17 |
| 16:00 | 4473 | Fiorentina vs Juventus | 2.84 | 3.03 | 2.51 |
| 16:30 | 1030 | VfL Bochum vs Werder Bremen | 2.80 | 3.46 | 2.30 |
| 16:30 | 1604 | Stuttgart vs Schalke 04 | 1.75 | 3.78 | 4.08 |
| 16:30 | 1685 | Bayer Leverkusen vs SC Freiburg | 1.87 | 3.71 | 3.61 |
| 16:30 | 1843 | VfL Wolfsburg vs FC Koln | 2.10 | 3.45 | 3.20 |
| 16:30 | 2214 | Union Berlin vs Bayern Munchen | 6.97 | 5.18 | 1.34 |
| 17:00 | 1393 | Ross County vs Aberdeen | 3.61 | 3.26 | 2.04 |
| 17:00 | 2010 | Tottenham vs Fulham | 1.45 | 4.49 | 5.99 |
| 17:00 | 2228 | Brentford vs Leeds | 2.10 | 3.49 | 3.14 |
| 17:00 | 3278 | Livingston vs Hearts | 3.27 | 3.27 | 2.16 |
| 17:00 | 3638 | Wolverhampton vs Southampton | 2.18 | 3.29 | 3.14 |
| 17:00 | 3829 | Chelsea vs West Ham | 1.49 | 4.31 | 5.61 |
| 17:00 | 4145 | Hibernian vs Kilmarnock | 1.67 | 3.62 | 5.02 |
| 17:00 | 5470 | Nottingham vs Bournemouth | 1.98 | 3.35 | 3.60 |
| 17:00 | 5758 | Newcastle vs Crystal Palace | 2.00 | 3.30 | 3.60 |
| 17:15 | 4132 | Real Madrid vs Betis | 1.41 | 4.97 | 6.29 |
| 17:15 | 5302 | Genoa vs Parma | 1.67 | 3.60 | 4.90 |
| 17:30 | 4079 | Porto B vs Vilafranquense | 1.79 | 3.54 | 4.09 |
| 17:30 | 4227 | Sporting Braga vs Vitoria Guimaraes | 1.38 | 4.73 | 7.24 |
| 17:30 | 4348 | Ajax vs Cambuur | 1.08 | 9.62 | 19.05 |
| 18:00 | 1530 | BSC Young Boys vs Stade Nyonnais | 2.65 | 3.59 | 2.25 |
| 18:00 | 2033 | AJ Auxerre vs Marseille | 4.43 | 3.93 | 1.68 |
| 18:00 | 2694 | Jong Sparta Rotterdam vs FC Volendam | 1.56 | 4.11 | 4.60 |
| 18:00 | 3615 | RB Salzburg vs WSG Wattens | 1.13 | 7.28 | 12.78 |
| 18:00 | 5706 | Maccabi Tel Aviv vs Ironi Kiryat Shmona | 1.30 | 4.80 | 8.04 |
| 18:30 | 2585 | FC Krasnodar vs Sochi | 2.69 | 3.49 | 2.37 |
| 19:00 | 3279 | FC Sion vs FC Basel | 2.82 | 3.37 | 2.36 |
| 19:00 | 3599 | Bodo Glimt vs Molde | 1.79 | 3.97 | 3.77 |
| 19:00 | 3752 | AC Milan vs Inter | 2.67 | 3.17 | 2.57 |
| 19:00 | 3762 | Doxa Katokopia vs Apollon Limassol | 4.76 | 4.00 | 1.64 |
| 19:15 | 3801 | Basaksehir vs Alanyaspor | 1.91 | 3.46 | 3.82 |
| 19:30 | 1433 | Aston Villa vs Manchester City | 7.06 | 4.83 | 1.37 |
| 19:30 | 4679 | Eintracht Frankfurt vs RB Leipzig | 3.35 | 3.65 | 1.97 |
| 19:30 | 5011 | Real Sociedad vs Atletico Madrid | 2.87 | 3.07 | 2.52 |
| 19:45 | 2611 | Twente vs PSV Eindhoven | 3.65 | 3.65 | 1.88 |
| 20:00 | 4781 | Lyon vs Angers | 1.28 | 5.62 | 8.43 |
| 21:00 | 3239 | Sparta Rotterdam vs FC Volendam | 1.60 | 3.96 | 4.91 |
| 21:30 | 3301 | FC Zurich vs FC Lugano | 2.16 | 3.50 | 3.05 |
| 21:45 | 3356 | Lazio vs Napoli | 2.80 | 3.35 | 2.35 |
| 21:45 | 4064 | Fenerbahce vs Kayserispor | 1.39 | 4.92 | 6.63 |
| 21:45 | 5347 | Standard Liege vs Oostende | 2.00 | 3.52 | 3.42 |
| 22:00 | 1863 | GO Ahead Eagles vs Feyenoord | 6.80 | 4.80 | 1.38 |
| 22:00 | 2797 | Nantes vs Paris St Germain | 8.20 | 5.47 | 1.30 |
| 22:00 | 4218 | Sevilla FC vs Barcelona | 4.06 | 3.53 | 1.85 |
| 22:30 | 4646 | Gil Vicente vs Porto | 6.42 | 4.41 | 1.44 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.


# MULTICHOICE YAAHIDI NEEMA KUIBEBA SANAA YA TANZANIA

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Multichoice Tanzania imeendelea kuishukuru serikali kwa kushirikiana nayo katika kuendeleza sekta ya sanaa hapa nchini.

Akizungumza katika hafla maalumu iliyoandaliwa na Multichoice Tanzania jana, Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi wa kampuni hiyo, Nehemia Mchechu, alisema kitendo cha Waziri wa Sanaa, Utamaduni na Michezo, Mohamed Mchengerwa, kushiriki katika hafla hiyo kimethibitisha serikali ipo nao kwa ajili ya maslahi mapana ya tasnia ya Sanaa, Utamaduni na Michezo.

"Tumeshaelezwa na tutaendelea kujuzwa kwa kuna ni nini tumefanya sisi MultiChoice katika kuleta mapinduzi katika tasnia ya Sanaa hapa nchini. Miradi kama ya mafunzo maalumu ya vijana wetu katika uzalishaji wa filamu kupitia program ya MultiChoice Talent Factory; kuongezwa kwa maudhui ya kitanzania katika kisimbuzi cha DStv, Kuanzishwa kwa chaneli mpya (Maisha Magic Poa), ambayo ni mahsusi kwa maudhui ya kitanzania; kuongeza wigo katika kutoa ajira kwa vijana wetu - yote hayo ni mambo ambayo tunayafanya kwa makusudi mapana ya kukuza uwezo wetu kama nchi kushiriki na kushindana vizuri katika soko la maudhui duniani," alisema Mchechu.

Aliongeza, kutokana na mchango wao huo, tayari wameshaanza kuona matunda ambapo hivi sasa filamu za wasanii wa Tanzania zimeanza kuingia katika tuzo mbalimbali za kitaifa na kimataifa na kuibuka kinara.

"Kwa mwaka 2022 tumeweza kutwaa tuzo kadha wa kadhaa ikiwamo Africa Magic Viewers Choice Awards, kupitia filamu ya Obambo, pia filamu zetu mbili mojawapo ikiwa imeandaliwa na mhitimu wa programu ya MultiChoice Talent Factory ziliweza kuibuka na ushindi wakati wa tuzo za Zanzibar International Film Festival (ZIFF), zilizofanyika mapema Juni mwaka huu visiwani Zanzibar," Mchechu alisema.

Aliongeza, Multichoice inaahidi itaendelea kutoa ushirikiano na kuimarisha uwekezaji katika sekta hiyo ya sanaa, utamaduni na michezo kwani hivyo ndivyo vyanzo vikuu vya maudhui yao.

Aliipongeza serikali kwa kuunda kamati maalum ya kufuatilia masuala ya hakimiliki. " Kwa hakika hili ni suala kubwa na tunatumaini maoni na ushauri uliotolewa na kamati utatumika katika kulitafutia ufumbuzi suala zima la wizi wa maudhui na ambao (Content Piracy) ni tatizo kubwa sana linalotishia ustawi wa sekta ya maudhui na utangazaji na ni janga kubwa sana kwa sekta ya sanaa." aliongeza mjumbe huyo.




Mkuu wa Idara ya Mauzo ya Kampuni ya Africarriers, Mohammed Ladha (katikati), akimkabidhi funguo ya basi walilopewa Simba Queens, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez kwa ajili ya usafiri wa timu hiyo. Kushoto ni wachezaji wa Simba Queens waliofika kushuhudia makabidhiano hayo. **PICHA: SAADA AKIDA**

# Makocha 300 waitaka Azam FC

**Na Adam Fungamwangogo**

MAKOCHA zaidi ya 300, wametuma maombi ya kazi ya kuifundisha Azam FC inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo hivi karibuni imetangaza kuachana na aliyekuwa Kocha Mkuu, Abdihamid Moallin, imefahamika.

Ofisa Habari wa Azam FC, Thabit Zacharia 'Zake', aliliambia gazeti hili jana pamoja na idadi hiyo ya makocha kuomba kazi, lakini hakuna hata jina moja la kocha mzawa.


"Tumeendelea kupokea maombi na wasifu wa makocha mbalimbali, hadi sasa tumepokea zaidi ya wasifu 300, lakini kwa bahati mbaya kati ya hao hakuna hata Mtanzania mmoja, hii inatutia shaka sana na kujiuliza wanaogopa nini, au sisi Azam hatuna viwango vya kufundishwa na Watanzania, wao wako juu sana kuliko sisi," alihoji Zaka.

Alisema, bado wanaendelea kupokea maombi huku akiwataka makocha wa Watanzania kuchangamkia fursa hiyo kama uthubutu wa makocha kutoka nje ya nchi unavyofanyika.

"Sisi hatukutoa tangazo lolote la kutaka watu walete wasifu, lakini makocha kutoka nje waliposikia tu tumeachana na kocha, wakaanza kumiminika kuleta, na hii ndiyo tabia ya watu wa mpira wa miguu, hawasubiri tangazo, wakiona tu kocha ametimuliwa," Zaka aliongeza.

Michezo
Jumamosi Septemba 3, 2022
Nipashe

UKURASA 21



**Aubameyang rasmi asajiliwa na Chelsea**



Beki wa Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), Fatma Issa 'FettyDensa' (kushoto), akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa Comoro katika mechi ya mashindano ya COSAFA iliyochezwa mjini Port Elizabeth, Afrika Kusini jana. Twiga Stars ilishinda mabao 3-0. **PICHA: TFF**

# Yanga yaamshwa, Simba yapata pigo

●●●Hata hivyo kila upande unaendelea kujiimarisha kwa ajili ya Ligi Kuu Bara na mechi za...

**Saada Akida na Shufaa Lyimo**

WAKATI Simba ikipata pigo kwa kumpoteza daktari wake, Yassin Gembe, nyota wa zamani wa Yanga, Sunday Manara 'Kompyuta' ameitaka klabu hiyo isibweteke kama inahitaji kutetea ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika watakayoshiriki.

Taarifa rasmi iliyotolewa na Simba imesema, Gembe amefariki jana mchana katika hospitali ya Taifa ya Rufaa ya Muhimbili ambapo alikuwa amelazwa.

"Kwa masikitiko makubwa tunatangaza kifo cha aliyekuwa daktari wa timu ya wanaume (Simba), ambaye kwa sasa alikuwa daktari wa timu ya vijana, Dk. Yassin Gembe, ambacho kimetokea leo (jana) mchana katika Hospitali ya Taifa ya Rufaa ya Muhimbili," ilisema kwa kifupi taarifa ya klabu hiyo.

Hata hivyo, wachezaji wa Simba na benchi la ufundi juzi walipata nafasi ya kwenda kumjulia hali ikiwa ni muda mfupi baada ya kurejea nchini wakitokea Sudan walipokwenda kushiriki mashindano maalumu.

Komputa aliliambia gazeti hili Yanga inatakiwa iongeze juhudi katika kila idara kwa ajili ya kuhakikisha wanafanya vizuri zaidi ya walivyofanikiwa katika msimu uliopita.

"Timu zote zimejiimarisha na kujipanga, ninawakumbusha Yanga wasibweteke, waongeze mazoezi, wajue ushindani umeongezeka katika michezo ya Ligi Kuu msimu huu na ile ya kimataifa watakayoshiriki," alisema Kompyuta.

Aliongeza licha ya mabosi wa klabu hiyo kufanya usajili mzuri lakini wachezaji wanapaswa kutambua wajibu wao wanapokuwa uwanjani.

"Nawakumbusha wachezaji wa Yanga watambue wana deni kubwa ambalo wanatakiwa wawalipe mashabiki wao, wanatakiwa kufanya vizuri katika michezo ya ligi ya nyumbani pamoja na mashindano ya CAF, kule ndio kuna ushindani halisi, waongeze bidii," alisema nyota huyo ambaye ni baba wa Haji Manara.

Aliongeza timu kufanya usajili mzuri haimaanishi imeshashinda mechi, wachezaji wanatakiwa wacheze kwa kuelewana na kwa umakini na vile vile kuwa na utulivu ndani na nje ya uwanja.

"Bila nidhamu timu haiwezi kufanikiwa, kuna mechi nyingi mbele yao, kuna wale watakaoumia, basi waliobakia watatakiwa kujituma na kuibeba timu hadi ifikie malengo yake, hakuna miujiza katika soka la sasa," alisema.

Aliongeza viongozi wa timu, wachezaji pamoja na mashabiki wanapokuwa na umoja na ushirikiano, ni rahisi kufikia malengo yaliyowekwa kwa sababu hakuna linachoshindikana.

"Nawatakia kila la kheri katika mashindano ya kimataifa ambayo wanatarajia kuanza hivi karibuni, waongeze tu umakini katika michezo hiyo, naamini watapeperusha vyema bendera ya timu yetu, tunawaamini," alimaliza.

Yanga inaendelea na mazoezi kwa ajili ya kuvaana na Azam FC katika mechi ya raundi ya tatu ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa Jumanne kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

## Stars kitaeleweka, Twiga mambo safi

**Na Saada Akida**

NINATAKA ushindi, hayo ni maneno ya Kocha Mkuu wa Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), Honour Janza, kuelekea mchezo wa marudiano wa kusaka tiketi ya kushiriki fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), dhidi ya Uganda utakaochezwa leo jijini Kampala.

Janza alisema amewaandaa wachezaji wake kucheza kwa mfumo tofauti na walivyoonekana katika mchezo wa kwanza sababu wao wanahitaji matokeo ya aina moja tu.

Kocha huyo alisema amewataka nyota wake wasiwe na hofu yoyote lakini wakiongeza umakini kwa ajili ya kuhakikisha wanafikia malengo na kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

"Wachezaji wako katika hali nzuri, wanaelewa tunachokihitaji, tunajua tuko nyuma, nimewataka waongeze bidii na uwezo wa kupata ushindi tunao," alisema Janza ambaye timu yake ilifunga bao 1-0 kwenye mechi ya kwanza.

Wakati huo huo, Timu ya Soka ya Taifa ya wanawake (Twiga Stars), imeanza vyema kutetea ubingwa wa mashindano ya COSAFA kwa kuwachapa Comoro mabao 3-0 dhidi ya Comoro katika mchezo uliochezwa jana mchana mjini Port Elizabeth.

Bao la kwanza la Twiga Stars lilifungwa na Donisia Minja dakika ya 13 baada ya kuunganisha krosi iliyopigwa na Mwanahamisi Omari 'Gaucho' huku la pili likiwekwa kimiani dakika yaa 41 na Enekia Kasonga.

Twiga Stars ilienda mapumziko ikiwa mbele kwa mabao 2-0 na goli lake la tatu dakika ya 50 likifungwa na Enekia ambaye aliibuka mchezaji bora wa mechi hiyo.

Mabingwa hao watetezi watashuka tena dimbani keshokutwa kucheza dhidi ya Botswana na watamaliza hatua ya makundi Septemba 7, mwaka huu kwa kuvaana na Malawi.

Kikosi cha Twiga Stars kilichoanza katika mchezo huo wa jana ni Zulfa Ally, Anastazia Katunzi, Violeth Nicholaus, Fatma Issa 'Densa', Diana Msewa, Irene Kisisa, Amina Bilali, Enekia Kasonga, Donisia

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >